# Nipashe


Alhamisi Juni 2, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580964

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




**Sabaya** afunguliwa mashtaka mapya uhujumu uchumi

UKURASA 2



HAZARD HAJUI HATIMA YAKE UBELGIJI KOMBE LA DUNIA

UKURASA 21



# UNYAMA

• **Hausigeli** adaiwa kumnyonga mtoto wa bosi, mume amjeruhi mke sehemu za siri... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**WANACHAMA, WAFUASI CHADEMA WAACHIWA HURU**

WANACHAMA na viongozi 19 wa Chama cha Demokrasia na...

UKURASA WA 5

**NAPE AONYA HUDUMA SIMU BILA RIDHAA**

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Nape Nnauye, ameiagiza Mamlaka ya...

## Samia aagiza viongozi maisha duni kunufaika TASAF

UKURASA 3

UHAKIKA UPATIKANAJI, BEI MAFUTA

GESI MAGARI, VIWANDA, MAJUMBANI. NEEMA; NISHATI MPYA, GESI ASILIA YAJA

EWURA, TANESCO, TPDC KUSUKWA

LINDI, KAGERA, KIGOMA, KATAVI KICHEKO

WAZAWA, SEKTA BINAFSI KAZI KWAO



UKURASA 3

Waziri wa Nishati, Januari Makamba, akiwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Dira mpya Nishati

MICHEZO NABI ATAJA WAKUSAJILI YANGA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6



Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya (kushoto), akiteta na Wakili wa Utetezi, Helena Makunda, baada ya kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi jana, kwa ajili ya kusomewa mashtaka saba yakiwamo ya kuendesha genge la uhalifu, kupokea rushwa, utakatishaji wa fedha pamoja na ukiukwaji wa Mamlaka ya Utumishi. **PICHA: MARY MOSHA**

# Vitendo vya kinyama vyatikisa

**Na Waandishi Wetu**

NI unyama. Ndiyo picha halisi inayoweza kuelezewa kutokana na matukio ya kikatili baada ya msichana wa kazi kudaiwa kumnyonga mtoto wa bosi wake mwenye umri wa miaka minane (jina linahifadhiwa) Kimara, Dar es Salaam.

Sambanba na tukio hilo, mkoani Mara, mwanamume mmoja amemjeruhi mke wake kwa panga sehemu za siri kwa kile alichodai kutaka kumkeketa baada ya kumtuhumu kuwa alikuwa akisaliti ndoa yao.

Tukio la binti wa kazi (jina limehifadhiwa) kunyonga, lilitokea juzi wakati wazazi na kaka wa mtoto huyo wakiwa kazini.

Baba Mzazi wa mtoto huyo ambaye ni daktari wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili Tawi la Mloganzila, Erick Kimaro, alisema baada ya kupata taarifa, walirudi nyumbani na kumkuta mtoto wao amelala huku sehemu ya shingoni ikiwa na alama ya vidole.

"Tumeona shingoni mwake kuna alama ya vidole na wekundu ambao ni dalili kuwa alikufa kwa kunyongwa," alisema akiongeza kuwa: "Historia yake hatuijui kwani rafiki wa mke wangu alituletea kutoka Tanga. Alikuja Jumamosi (Mei 28) na Jumatatu (Mei 30) tukio la mauaji lilitokea."

Mama mzazi, ambaye pia ni daktari na Mratibu wa Magonjwa Yasiyoambukiza mkoani Dar es Salaam, Digna Siriwa, akisimulia mkasa huo, alisema walipoingia ndani walimkuta mtoto amelala chali huku mdomo wake ukiwa wazi na umebadilika rangi ni kuwa mweusi.

"Uso wake ulikuwa umevimba na kuwa mweupe sana, sehemu ya paji la uso kuna alama ya kuvilia damu. Tulipomgusa kichwa chake kilikuwa baridi. Kuanzia shingoni hadi miguuni alikuwa wa moto na mdomo wake kauacha wazi kama alikuwa akitafuta hewa," alisema Dk. Siriwa.

Ansila Kimaro ambaye ni mmoja wa ndugu wa marehemu, alisema alikuta mtoto akiwa amefariki dunia lakini glovu ziko mdomoni. Alisema alijaribu kuhoji kama mauaji hayo yamefanywa na mfanyakazi wa ndani au la.

"Nilijibiwa na mama yake kuwa mfanyakazi wa ndani yupo lakini anajibu mambo yasiyoeleweka pale anapoulizwa mazingira ya kifo cha mtoto wake," alisema Ansila huku akibainisha kuwa kipindi chote wanahangaika na mtoto huyo, mfanyakazi huyo alikuwa ndani na hakuonekana kuwa na dalili yoyote ya kukimbia hadi alipokamatwa na polisi.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, amethibitisha kutokea tukio hilo na kwamba uchunguzi unafanyika.

**AMJERUHI MKEWE**

MKAZI wa Serengeti mkoani Mara, Gimusi Murimi (42), anadaiwa kumwingizia panga mkewe sehemu za siri kwa kile alichodai ni kumkeketa, ili kumdhibiti kuchepuka na wanaume wengine.

Taarifa za uhakika kutoka kwa ndugu zinasema mwanamume huyo alilenga kumpanua miguu mke wake amkekete kwa kutumia panga kama namna ya kumdhibiti kuwa na wanaume wengine.

Ndugu hao ambao hawakutaka kutaja majina yao, walisema Murimi baada ya kufanya tukio hilo alitoroka kwa kuwa aliwatishia kwa sime watu waliotaka kumkamata. Chanzo cha ugomvi huo kwa wanandoa hao ni baada ya mwanamme kumtuhumu mke wake kuchepuka wakati yeye akiwa hayuko nyumbani.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mara, Longinus Tibishubwamu, alithibitisha mtuhumiwa huyo kushikiliwa kwa mahojiano zaidi na kwamba uchunguzi wa awali ulibaini anafanya kazi mji wa Katoro mkoani Geita na kwamba hurudi nyumbani kuisalimia familia yake mara kwa mara.

Pia ulibainі alirudi nyumbani kwake Mei 25, mwaka huu, alidai kubaini mkewe si mwaminifu kwenye ndoa, ndipo alimshambulia kwa fimbo na baadaye kumwingizia panga sehemu za siri na kumjeruhi. Mwanamke huyo anaendelea na matibabu katika hospitali.

**ALIYEUA MKE**

Mwili wa Said Oswayo, aliyemuua mkewe kwa risasi saba naye kujipiga risasi moja kidevuni, ulisafirishwa jana kutoka mwanza kwenda mkoani mara kwa maziko.

Mwili wa Oswayo uliagwa jana katika chumba cha kuhifadhia maiti cha Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando na kupelekwa nyumbani kwake, Buswelu kabla ya kupelekwa kijiji cha Etaro wilayani Musoma.

Aidha, mwili huo ulipofika nyumbani kwake, haukuingizwa ndani ya nyumba na kubaki ndani ya gari aina ya Toyota Coaster huku waombolezaji wakiingia ndani ya nyumba kufanya majadiliano kabla ya kuanza safari hiyo.

Akizungumzia suala la mwili kutoingizwa ndani, mlezi wa familia ya Oswayo, Chambi Lukonga, alisema hawakufanya hivyo kwa kuwa walikuwa wanapita kwenda mkoani Mara kwa maziko.

Mwili wa Oswayo uliokotwa juzi kandokando ya Ziwa Victoria, jijini Mwanza ukiwa na majeraha ya risasi siku chache baada ya kumuua mke wake, Swalha.

**Imeandikwa na Moshi Lusonzo (Dar) na Richard Makore (Mwanza)**

# Sabaya afunguliwa kesi mpya uhujumu uchumi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

ALIYEKUWA Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, na wenzake wanne, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi mkoani Kilimanjaro akikabiliwa na mashtaka saba ya uhujumu uchumi.

Mashtaka hayo ni pamoja na kuongoza genge la uhalifu, utakatishaji wa fedha, kuomba na kupokea rushwa na ukiukwaji wa maadili ya utumishi.

Mapema June mosi mwaka huu majira ya 11;36 asubuhi, Sabaya alifikishwa katika viwanja vya mahakama mjini hapa jana saa 11:36 asubuhi chini ya askari kanzu wenye mitutu ya bunduki wakiongozwa na gari aina ya Toyota Landcruisrer na kufuatiwa na Toyota Hiace yenye vioo vyeusi lililokuwa limembeba pamoja na wenzake.

Kesi hiyo namba 2/2022 uhujumu uchumi, mbali na Sabaya, wengine ni Sylvester Nyegu, John Aweyo, Nathan Msuya na Antoro Assey , mshtakiwa wa tano hakufikishwa mahakamani na hakuna maelezo yaliyotolewa.

Baada ya kuingizwa mahakamani, watuhumiwa walikaa kwa dakika 11 kabla ya hakimu kuingia huku mshtakiwa namba moja (Sabaya) akionekana kuwa na macho mekundu.

Akisoma mashtaka mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Salome Mshasha, Wakili wa Serikali Mkuu, Tumaini Kweka, alidai kuwa shtaka la kwanza linawakabili watuhumiwa wote na kwamba Februari 2, 2021 washtakiwa waliongoza genge la uhalifu katika wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro.

Katika shtaka la pili, Kweka alidai kuwa linamkabili Sabaya na kwamba Februari 21, 2021 aliomba rushwa ya Sh. milioni 30 kutoka kwa Godbless Swai katika eneo la Bomang'ombe, Hai mkoani Kilimanjaro.

Shtaka la tatu, Kweka alidai kuwa ni la kuomba na kupokea rushwa kwamba Sabaya alijipatia rushwa ya Sh. milioni 30 kutoka kwa Elibariki Swai kwa nia ya kuzuia taarifa za uchunguzi zilizohusiana na ukwepaji wa kodi.

Wakili Kweka alidai kuwa katika shtaka la nne na tano liliwakabili washtakiwa wa pili, tatu, nne na tano ambalo ni kumsaidia mshtakiwa namba moja, Sabaya, kushawishi na kujipatia manufaa asiyostahili ya Sh. milioni 30 kutoka kwa Alex Swai huku akijua ni kinyume cha sheria.

Pia alidai kuwa shtaka la sita linamhusu Sabaya kuhusu ukiukwaji wa maadili ya utumishi akiwa mtumishi wa umma katika wilaya ya Hai na shtaka la saba ni utakatishaji wa fedha ambao unawakabili watuhumiwa wote.

Baada ya upande wa mashtaka kuwasilisha hoja hizo, wakili wa utetezi Helena Makunda alieleza kutoridhika na mwenendo wa shauri hilo katika mahakama hiyo kwa kile alichodai ni kukosekana kwa kibali cha moja kwa moja kutoka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Moshi kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha.

"Hatujaridhishwa na mwenendo wa mahakama ulivyofanyika. Mawakili wa utetezi hawakupewa taarifa na pia hakuna kibali cha moja kwa moja kilichotokea katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi kwenda Arusha kwa ajili ya watuhumiwa kufika katika mahakama ya Moshi ili kusomewa mashtaka yao," alidai.

Hoja hiyo iliibua mzozo wa kisheria uliochukua takriban dakika saba na sekunde 35, hatua iliyosababisha Hakimu Mshasha kuahirisha shauri hilo kwa takribani dakika 15 ili kutatua mzozo huo.

Baada ya hapo, Hakimu Mshasha alisema mwenendo wa kesi hiyo uko sahihi kutokana na upande wa Jamhuri kuwasilisha kesi hiyo mapema Mei 30, 2022 kwa kufuata taratibu zote ikiwamo kuandika kibali kwa Mkuu wa Gereza la Kisongo, Arusha.

"Nimepitia kesi hii ililetwa hapa Mei 30 na baada ya hapo tukajulishwa kwamba washtakiwa wako katika gereza la Kisongo. Kiliandikwa kibali cha kuwataka wafike mahakamani hapa baada ya kukamilisha kesi iliyokuwa inawakabili Mei 31 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha.

"Mahakama haina jukumu la kumweleza wakili wa utetezi juu ya kesi kwa maana haina taarifa nao, hivyo ni jukumu la mshtakiwa kuwapa taarifa wawakilishi wao. Kwa hiyo hoja ya wakili wa utetezi haina mashiko na inatupiliwa mbali," alisema Mshasha huku akisema kesi hiyo itafikishwa tena Juni 7, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa kabla ya kuendelea kusikilizwa.

Hata hivyo, akiwa anatiririkwa na machozi, Sabaya alieleza mahakamani kutokuwa na imani na Wakili Kweka kwa madai kuwa ana chuki na visasi.

"Nina imani kubwa na mahakama hii. Nina imani kubwa na ofisi ya mwendesha mashtaka lakini sina imani hata kidogo na Kweka kwa kuwa ameletwa hapa kuhakikisha ananifunga. Ana chuki moyoni, ana visasi ikizingatiwa kuwa anatoka kwenye wilaya nilikokuwa nafanya kazi.

Namwomba Rais Samia Suluhu Hassan aingilie kati suala hili ili nitendewe haki na kurejea nyumbani kwa ajili ya kuhudumia familia yangu pamoja na watoto wanaonitegemea," alidai Sabaya huku akifuta machozi.

## HABARI KITAIFA



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama (kulia kwake), akikagua sehemu ya magari 241, kabla ya kuyakabidhi kwa mamlaka za maeneo ya utekelezaji kwa shughuli za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), kwa Tanzania Bara na Zanzibar, katika viwanja vya Posta, Kijitonyama, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Dira mpya sekta ya Nishati

**Na Romana Mallya, DODOMA**

WAKATI jana kuliwasilishwa bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka ujao wa fedha ikihitaji Sh. trilioni 2.905, jambo la awali linalokaribisha tabasamu ni kushuhudiwa nyongeza ya zaidi ya Sh. bilioni 510, kutoka Sh. trilioni 2.386 ambazo matumizi yake yanaishi mwezi huu.

Ndani ya makadirio hayo ya tabasamu, kuna sura kuu tatu ambazo zote zina tafsiri ya kumkomboa na kumnyanyua Mtanzania katika maisha yake na matumizi ya nishati, yakilenga kwenye maeneo: Kuleta mapinduzi katika teknolojia ya sekta hiyo.

Mengine yanahusu maboresho ya kina kwenye miradi ya teknolojia inayotumika katika nishati nchini, kuzisuka upya taasisi zinazosimamia shughuli za nishati, na kuendana na dunia kuendesha miradi kisomi, ikiwamo kufanyika utafiti, hali kadhalika kuibua nishati mpya na matumizi yake.

Hapo ndipo patafanya kushuhudiwa rasmi kuanzia mwezi ujao, Tanzania inayotumia gesi yake kwenye magari ya serikali na binafsi, viwandani na majumbani; huku nishati jadidifu ikiibuliwa; bei isiyotetereka na akiba ya kutosha ya petroli, wadau wake bandari za Tanga, Dar es Salaam na Mtwara wakifanya kinachotakiwa na wananchi.

**SALAMU ZA WAZIRI**

Akiwasilisha jana bungeni jijini hapa makadirio hayo, Waziri wa Nishati, January Makamba, alivitaja vipaumbele vyao 12 katika mwaka wa fedha 2022/23 vinavyojumuisha: Kutekeleza miradi mbalimbali ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme ikiwamo kupeleka umeme wa Gridi ya Taifa kwenye mikoa ya Katavi, Kigoma na Kagera na mradi mkubwa wa kuimarisha gridi hiyo.

Waziri huyo alisema vipaumbele vingine ni: Utekeleza miradi ya nishati vijijini pamoja na kuanza utaratibu wa kupeleka umeme katika vitongoji vyote nchini; ukamilisha mazungumzo ya mradi wa LNG Lindi na kuanza maandalizi ya utekelezaji wake; kutekeleza miradi ya nishati jadidifu ikiwamo jotoardhi, tungamotaka, upepo na jua pamoja na matumizi bora ya nishati.

Vingine ni kuhakikisha kunakuwapo na upatikanaji wa mafuta ya kutosha nchini, uanzishwaji wa hifadhi ya kimakakati ya mafuta na Mfuko wa Kudhibiti Mabadiliko ya bei zake; kuiimarisha TPDC na kampuni zake tanzu; kuboresha miundombinu ya kupokea, kushusha, kuhifadhi na kutoa mafuta katika Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara na maghala ya dhamana ya forodha.

Pia kuimarisha utendaji wa taasisi za wazawa hasa TANESCO, EWURA, na PBPA na huduma zinazotolewa; kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji wa sekta ya nishati; kuhakikisha ushiriki wa wazawa katika shughuli za nishati; kufufua shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia; na kuongeza matumizi ya nishati ya gesi kwa kupikia (LPG) na kwenye magari na viwanda (CNG).

**DAWA KUKATIKA UMEME**

Waziri January alisema serikali imetafuta mwarobaini wa kadhia hiyo, akifafanua kuwa kwa kiasi kikubwa kunatokana na uchakavu na kutotosheleza kwa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji umeme na wizara imekuja na mradi wa kuimarisha gridi ya taifa.

Alisema mradi huo ambao utatekelezwa kwa miaka minne utahusu uimarishaji wa miundombinu ya ugavi wa umeme katika mikoa mbalimbali ikiwa ni pamoja na ufungaji wa mitambo vifaa vya kisasa, ubadilisha wa nguzo za kiti kwa kusimika za zage, ufungaji wa nyaya zenye uwezo wa kusafirisha umeme mkubwa pamoja na mashine umba.

Alisema mradi huo utagharimu Dola za Marekani bilioni 1.9 (sawa na Sh. trilioni 4.420) na katika mwaka wa fedha ujao Sh. bilioni 500 zimetengwa kwa ajili ya kuanza. "Mradi utahusisha kununua na kufunga mashineumba 6,000, kununua na kusimika nguzo za njia za kusafirisha umeme 380,000, kununua na kufunga mita za luku 700,000, kujenga vituo vya kupooza umeme 14 za 220/33Kv na 132/33Kv, kununua na kufunga mashineumba kubwa 27 na kujenga njia za kusafirisha umeme za urefu wa kilometa 948 za msongo wa Kv132 na Kv220," alisema.

**NISHATI VIJIJI**

Waziri huyo alisema serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) itaendelea kutekeleza miradi ya kusambaza nishati bora vijijini na kuhamasisha matumizi yake.

"Serikali imesikia kilio cha muda mrefu cha wananchi kuhusu maeneo ya mjini yenye sifa zinazolingana na vijijini huku wakilipa bei ya kuunganishiwa umeme ya mjini, timu ya TANESCO na REA inazunguka katika miji yote kwa kuwashirikisha wabunge na yatajumuishwa kwenye bei za vijijini ya Sh. 27,000 na mchakato huu utakamilika ndani ya miezi sita," alisema.

**GESI MAJUMBANI**

Waziri January alisema TPDC inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia yenye urefu wa kilometa 10.04 kutoka bomba kubwa la kusafirisha gesi hadi eneo la bomba kubwa la kusafirisha gesi hadi eneo la Mnazi Mmoja ili kuwezesha matumizi katika maeneo hayo na kazi inatarajia kuanza Julai mwaka huu na kukamilika Februari mwakani na itagharimu Sh. bilioni 5.49.

Alisema serikali imepanga kujenga vituo vya kujaza gesi asilia iliyoshindiliwa kwenye magari katika Bohari Kuu za mafuta za serikali za Dar es Salaam na Dodoma ambapo kwa kuanzia magari ya wizara hiyo na taasisi zake yatafungiwa mfumo huo na Sh. bilioni moja zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za awali za mradi huo.

# Rais ataka viongozi wanaoishi maisha duni wanufaike TASAF

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu ameagiza viongozi wa vyama vya siasa wanaoishi katika mazingira duni wasizuiwe kunufaika na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kwa kuwa vyeo walivyonavyo sio kigezo cha kuwa na hali nzuri kimaisha.

Aliyasema hayo jana katika hafla ya kukabidhi magari 123 kati ya 241 kwa wakurugenzi wa halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za TASAF iliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Alisema kuwa viongozi hao hawakuchaguliwa kwa kigezo cha maisha bora bali kwa busara, heshima na imani waliyokuwa nayo wananchi wa maeneo yao.

"Kwa hiyo kama watu wamemchagua kuwa ndiyo kiongozi wao wa eneo lile isimzuie kufaidika na mpango huo wa TASAF. Kama vigezo vyote vinaonyesha kuwa anaishi kwenye mazingira duni, basi isimzuie kunufaika na mpango huo," alisema Rais.

Alisema serikali imeendelea kufanya maboresho kuhakikisha wananchi wanaoishi katika mazingira duni wanapata mahitaji yao ya msingi kupitia programu mbalimbali ikiwamo utoaji wa mikopo isiyo na riba na kutoa ruzuku kwa kaya zinazoishi katika mazingira duni kupitia TASAF.

"TASAF imekuwa taswira ya serikali katika kuwajali wananchi wake na kuwafikia katika maeneo yote Tanzania Bara na Zanzibar ili kuwatoa katika lindi la umaskini," alisema.

Vile vile, alisema serikali inafarijika kuona lengo la kuwakwamua Watanzania katika umaskini linafikiwa kwa kuwa taarifa zinaonyesha kuwa hadi kufikia mwaka huu mpango wa TASAF umesaidia kupunguza umaskini wa mahitaji ya msingi ya kaya kwa zaidi ya asilimia 10, huku umaskini uliokithiri kwa zaidi ya asilimia 12.

"Kabla sijaja hapa kwenye jukwaa hili nilipita kuona maonyesho ya wanufaika wa TASAF. Nimeshuhudia kwa macho watoto waliotoka kwenye mazingira duni na leo wameweza kufikia kiwango cha kusoma katika chuo kikuu," alisema.

Aliwaagiza watumishi hao licha ya kuwapa fedha wananchi, wawape elimu ya kutumia rasilimali walizonazo ili kuwatoa katika maisha duni wanayoishi na kutimiza Malengo ya Maendeleo Endelevu ya dunia (SDG's) linalowataka kufanya shughuli za maendeleo bila kumwacha mtu nyuma.

"Lakini kuna mwananchi ana uwezo mkubwa sana, anaishi kwenye mazingira yasiyoridhisha, ana ng'ombe 200 -300...naomba sana mbali na kazi mnayofanya, fanyeni kazi ya elimu, kuwatoa watu kwenye umaskini wa fikra na waishi maisha yanayoeleweka," alisisitiza.

Aliwahimiza watumishi wa mfuko huo wazitumie shilingi trilioni mbili zilizoko TASAF kwa malengo yaliyokusudiwa kwa sababu ni fedha za mkopo nafuu uliochukuliwa kuzikwamua familia duni.

Alitoa wito wa Wakurugenzi na Waratibu wa TASAF kusimamia magari hayo ili yatumike kwa shughuli zilizokusudiwa badala ya kufanyia biashara, kubeba mikaa, nazi, abiria au kuendea shamba.

Kuhusu mafanikio ya mpango huo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, alisema TASAF awamu ya tatu sehemu ya pili imefikia kaya zenye uhitaji 1,279,325 katika vijiji, shehia na mitaa 16,104 sawa na Watanzania zaidi ya milioni sita.

Waziri wa Nchi, Ofisi wa Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar, Hamza Hassan Juma, alisema mradi huo unatekelezwa kwenye shehia 388 kwa kuwapatia fursa na kuwezesha kukidhi mahitaji yao ya msingi ikiwamo chakula, elimu na afya.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

**YAH: SHAURI NA. 86 LA 2019**

**MAWENI LIMESTONE LTD.......................................................MDAI**

**DHIDI YA**

**FRANCIS THEOPIL NGOWI..........................................MDAIWA WA KWANZA**
**ESTER ELIA MATERU..........................................MDAIWA WA PILI**
**HADIJA ATHUMAN MWAMBASHI..............................MDAIWA WA TATU**
**ABDALLAH PASCAL MZIRAI..................................MDAIWA WA NNE**
**LUVI JOHN PATRICK..........................................MDAIWA WA TANO**
**GODFREY JOHN PATRICK....................................MDAIWA WA SITA**
**AMIRI MAJATA..................................................MDAIWA WA SABA**
**MGETA STANLEY...............................................MDAIWA WA NANE**
**GERALD ALEX MALIGA........................................MDAIWA WA TISA**
**OMARY MJATA..................................................MDAIWA WA KUMI**

**KWA: LUVI JOHN PATRICK, GODFREY JOHN PATRICK, AMIRI MAJATA, MGETA STANLEY, GERALD ALEX MALIGA, OMARY MJATA – POPOTE ULIPO**

**MAWENI LIMESTONE LTD,** amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Tanga. Shauri husika limepangwa kusikilizwa tarehe 2/6/2022 saa tano kamili asubuhi (5:00). Hivyo basi, unatakiwa kuleta utetezi wako ndani siku 21 kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Tanga. Endapo hutatekeleza haya, shauri hili litasikilizwa upande mmoja na Hukumu kutolewa dhidi yako.
**AMRI** hii imetolewa na kutiwa Saini Muhuri/Lakiri wa Baraza hili leo tarehe 30/5/2022.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
TANGA

116883102

# Wanachama, wafuasi CHADEMA waachiwa huru

**Na Richard Makore,** MWANZA

WANACHAMA na viongozi 19 wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) waliokamatwa kanisani wakimwombea mwenyekiti wao, Freeman Mbowe, na kufikishwa mahakamani jijini Mwanza, wamefutiwa mashtaka dhidi yao.

Kesi hiyo namba 77 ya mwaka 2021, ilifutwa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza baada ya kukaa mahabusu miezi 10.

Wanachama hao walikamatwa Agosti 15, mwaka jana, katika Kanisa Katoliki la Kawekamo Jimbo Kuu la Mwanza kwa madai ya kufanya fujo kwa waumini.

Kesi hiyo ilikuwa mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza, Bonaventure Lema, na tayari washtakiwa walikuwa wamesomewa mashtaka yao. Wanachama hao, Aprili 13, mwaka huu, walisomewa maelezo ya awali ya kesi yao mahakamani hapo na kukana huku upande wa mashtaka ukiahidi kupeleka mashahidi saba wakiwamo viongozi wa Kanisa Katoliki Parokia ya Kawekamo na vielelezo vinne vya ushahidi.

Washtakiwa hao kwa pamoja walikuwa wakikabiliwa na madai ya kufanya ghasia katika mkutano wa dini uliofanyika katika kanisa hilo Agosti 15, 2021 na kusababisha waumini washindwe kusikiliza neno la Mungu. Wanachama hao pamoja na viongozi wa mikoa na kanda kwa pamoja walikana mashtaka hayo mnamo Agosti 19 mwaka jana.

Makada hao wa CHADEMA walidaiwa kufika kanisani hapo kwa ajili ya kumwombea Mbowe ambaye alikuwa mahabusu kwa kesi ya ugaidi. Wafuasi hao ambao walikuwa nje kwa dhamana tangu mwaka jana, jana walifika tena katika mahakama hiyo kwa ajili ya kusikiliza ushahidi wa shauri lao.

Washtakiwa hao walikuwa wakitetea na wakili, Erick Muta na kesi imefutwa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kwa madai kuwa upande wa jamhuri hauna haja ya kuendelea nayo.

Wakili wa serikali, Emmanuel Luvinga, aliiambia mahakama hiyo kuwa Jamhuri haina haja ya kuendelea na kesi, hivyo wanachama hao waachiwe huru.

Tangu Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani wafuasi na wanachama mbalimbali waliokuwa na kesi za kisiasa walifutiwa.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizindua zoezi la upandaji wa miti katika Mji wa Serikali, Mtumba jijini Dodoma, jana. Kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka. **PICHA: OWM**

# Chongolo awageukia viongozi tatizo la tembo

**Na Maulid Mmbaga**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ameitaka Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na viongozi waliopewa jukumu la kuwasimamia wananchi Wilaya ya Meatu mkoani Simiyu, kuachia ngazi kama wameshindwa kutatua tatizo la tembo wanaosababisha kero kwa wananchi.

Wananchi wa wilaya hiyo wamekuwa katika taharuki kwa miaka mitatu sasa tangu tembo wanaotoka katika Pori la Akiba la Maswa waanze kuingia katika mashamba yao, huku wakitajwa kusababisha uharibifu wa mazao na udhorotaji wa shughuli za maendeleo.

Aidha, Rais Samia Suluhu Hassan, Februari 4, mwaka huu ikiwa imepita miezi mitatu alipopita kuelekea mkoani Mara, alitoa maelekezo kwa wizara husika kuchukua hatua za haraka kudhibiti tatizo hilo jambo ambalo mpaka sasa halijatatuliwa, huku wananchi wakiendelea kulilalamikia.

Wakati Chongolo akizungumza na wananchi wilayani hapo jana, alisema sio sawa kwa kiongozi kuacha kutatua matatizo yanayowakabili wananchi huku akieleza kuwa ni dharau pia kwa aliyewaagiza.

"Ndani ya wiki nne lazima viongozi wa Maliasili waje hapa wawaambie hatua wanazokuja kuzichukua kwa ajili ya kukabiliana na changamoto ya tembo kwa wananchi.

"Nyinyi ni waungwana mnawaona tembo mnawaacha, wanasumbua kwenye mazao, kwenye makazi yenu, kwa uungwana wenu mnawaacha kwasababu mnajua umuhimu wake, lakini mnachotaka ni kusaidiwa kuzuia madhara ya tembo kwenye shughuli zenu, na hilo watu wa mamlaka hawafanyi sio sawa," alisema Chongolo.

Aliahidi kuwa atalifikisha suala hilo katika ngazi za juu, akisisitiza kuwa hawawezi kuwa wanafanya masihara katika mambo yenye msingi, huku akiwataka viongozi kuwajibika kutokana na dhamana waliyopatiwa kwa kuwatumikia wananchi.

"Wananchi hawawezi wakawa wana kilio hakifiki mwisho, wamelalamika leo, kesho na jana, halafu tumekaa kwenye ofisi, tutaenda kuzungumza nao tuambiwe sababu za msingi za kuona jambo hilo sio la msingi, sipo tayari kuona hilo jambo linaendelea," alisema Chongolo.

"Rais anahangaika kuwaletea wananchi mbegu na mbolea ili walime zaidi, tembo wanakuja watu wa maliasili wanaagizwa waje washughulike kuweka mpango wa kudhibiti hawaji wanaacha nguvu inayotumika na wananchi ipotee bure hiyo sio sawa," alisema Chongolo.

"Hili litaenda kukoma sasa, tutaenda kuzungumza huko tukubaliane wako tayari kufanya wafanye hawako tayari wampe fursa mwenyekiti wa chama chetu kuweka watu ambao wako tayari kumsaidia kutatua changamoto za wananchi," alisema Chongolo.

Mwananchi wa eneo hilo Mussa Chami, ambaye ni mmoja wa waathirika wa tatizo hilo, alisema kilio cha tembo kimekuwa tatizo kubwa kwa wananchi wa wilaya hiyo, akidai kuwa limeleta shida katika utekelezaji wa shughuli zao za maendeleo.

Alisema shughuli nyingi za uchumi zimesimama katika eneo hilo kwasababu wanafanya kazi kwa muda mfupi kwa kuhofia wanyama hao, huku wakimwomba Rais Samia kuwasaidia kusimamia suala hilo ili litatuliwe.

"Tunaumia, tunamaliza mazao yetu kwa ajili ya hawa wanyama, wananchi wengi kwa sasa wamekuwa vilema, watu hawalali usiku na hawafanyi kazi kwa ajili ya tembo, wanalima mazao yao yanaliwa na wanyama hawa hakuna anayetufidia nguvu zetu zinapotea bure," alisema Chami.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Meatu, Dakawa Msoleni, akizungumzia suala hilo, alisema kumekuwa hatua mbalimbali ikiwamo kutoa elimu kwa wananchi wanaopakana na yenye uvamizi wa tembo.

"Kwa wale ambao wako karibu na Pori la Akiba ya Maswa, tumetoa elimu na vifaa vya kujihami kama matarumbeta na tumegawa tochi kwa ajili ya kufukuzia tembo na baadhi ya vitendea kazi vingine ambavyo kimsingi vimekuwa msaada kwenye jamii hiyo.

"Pia, kwasababu tatizo ni kubwa tumelipeleka ngazi za juu kama ambavyo Katibu Mkuu wa CCM ameahidi kulipeleka huko ili kulifanyia kazi, kwa hiyo nina amini litakuwa sawa," alisema Msoleni.

Kaimu Ofisa wa Wanyamapori Wilaya ya Meatu, Deusdedith Martini, alisema hatua za haraka walizozichukua hadi kufikia sasa kutatua tatizo hilo ni kuongeza askari wa wanyamapori kutoka vituo vingine ili kuongeza udhibiti, huku akiahidi wataendelea kudhibiti sambamba na kutoa elimu kwa wananchi.

# PM atoa maelekezo 8 kufanyika mji wa kijani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ametoa maelekezo nane ya masuala ya upandaji miti kwenye Mji wa Serikali ili kuwa na mandhari ya kuvutia na kukidhi dhana ya kuwa na Mji wa kijani.

Akizungumza jana kwenye uzinduzi wa programu ya upandaji miti katika Mji wa Serikali, Majaliwa alisema programu ya upandaji miti katika mji huo imeanza kutekelezwa kikamilifu kama ilivyoainishwa katika Mpango Kabambe wa Mji wa Serikali ambayo ni sehemu ya Mpango Kabambe wa Jiji la Dodoma wa mwaka (2019 - 2039).

Alisema mpango huo utafanya Mji wa Serikali kuwa wenye mandhari ya kuvutia, wa kisasa na utakaokidhi dhana hiyo huku usanifu na ubunifu wa majengo yanayoendelea kujengwa ukizingatia suala hilo.

Majaliwa alimwagiza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kwa kushirikiana na timu ya wataalamu wanaoratibu na kusimamia ujenzi wa Mji wa Serikali wahakikishe programu za upandaji miti unafuata Mpango Kabambe wa Mji wa Serikali na michoro iliyoidhinishwa ili kutokinzana na ujenzi wa miundombinu yote itakayojengwa na inayoendelea kujengwa.

"Pia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kwa kushirikiana na timu inayosimamia na kuratibu ujenzi wa Mji wa Serikali ikiwamo Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) na Idara ya Mazingira iliyoko chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, wahakikishe miti ya aina mbalimbali inapandwa na kutunzwa katika maeneo yote yaliyoainishwa na kuhakikisha mifumo ya umwagiliaji inafungwa mapema iwezekanavyo," alisema.

Alitaka kila wizara ihakikishe kuwa miche inayopandwa inatunzwa, inamwagiliwa hususan wakati wa kiangazi ili ikue vizuri.

"Pia ifanyiwe usafi ili kuondoa magugu yanayoweza kusababisha miche kufa. Tunataka mwakani kipindi kama hiki tupate kujionea matokeo ya kazi hii nzuri tunayoifanya leo," alisema.

Majaliwa aliziagiza taasisi zote zinazohusika na ujenzi wa miundombinu katika mji huo zikamilishe haraka taratibu na maandalizi yote ya kuanza kwa ujenzi wa miundombinu ya kudumu ya huduma zake na ofisi yake ipate mrejesho wa hatua za maandalizi ifikapo Juni 6, 2022.

"Timu ya wataalamu inayoratibu na kusimamia ujenzi wa Mji wa Serikali kwa kushirikiana na TFS na TARURA iwasilishe taarifa za mara kwa mara kuhusu utekelezaji wa programu za upandaji miti katika Mji wa Serikali," alisema.

Aidha, aliitaka Wizara ya Fedha na Mipango kuharakisha upatikanaji wa mahitaji ya fedha za miundombinu mbalimbali inayoendelea kujengwa na itakayojengwa ikiwamo kusimamia na kuratibu hatua za ununuzi ili kurahisisha utekelezaji wake.

"Wataalamu waelimishe jamii upandaji bora wa miti kwa kuzingatia hali ya hewa ya eneo husika ili upandaji uwe na tija. Kumekuwa na jitihada nyingi sana za upandaji miti, nisisitize miti ipandwe kwa kuzingatia ushauri wa wataalamu wetu," alisema.

HABARI KITAIFA

# Shaka aagiza mahindi bei nafuu kupelekwa Lindi

**Na Beatrice Shayo**

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, ameiagiza Wizara ya Kilimo kupeleka mahindi mkoani Lindi, yatakayouzwa kwa bei nafuu ukiwa ni mkakati wa kukabiliana na upungufu wa chakula.

Akizungumza na wananchi waliohudhuria uzinduzi wa ugawaji pembejeo za kilimo uliofanyika katika Kijiji cha Chingunduli, Kata ya Chiola, wilayani Nachingwea mkoani humo, alisema serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, imeanza kuchukua hatua.

"Naielekeza Wizara ya Kilimo kuleta mahindi kuja kuwauzia wananchi kwa bei nafuu hapa Lindi na bahati nzuri tukiwa na Mkuu wa Mkoa tumeshazungumza na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe na amekubali hilo jambo na analeta watu wake ili waje kufanya tathmini ya mahindi," alisema.

Aliongezea kuwa "Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Talek, ataongoza jopo kuhakikisha mahindi yanakuja Nachingwea. Rais Samia anajali watu wake anathamini watu wake, lakini ana mapenzi ya dhati kabisa kutatua changamoto hizi zinazowagusa ninyi moja kwa moja."

Alisema maelekezo ya Rais Samia baada ya kumwambia hali halisi aliwajulisha hawezi kuacha wananchi wake wafe na njaa watapeleka mahindi yenye bei nafuu, ili kuendesha maisha yao na kupata chakula cha uhakika.

Katika hatua nyingine Shaka, amezungumzia changamoto ya wanyamapori wakiwamo tembo kuwa tishio kwa wananchi wa Wilaya ya Nachingwea na Mkoa wa Lindi kwa ujumla na hiyo imetokana na uwapo wa idadi kubwa ya mifugo kama ng'ombe na mbuzi kwenye maeneo ya misitu na mapori.

"Wanyama ni wengi kuliko mahitaji ya hayo maeneo, kwenye mbuga na misitu huko kote sasa hivi kumeingiliwa, mkoa huu una wanyama wengi kuliko mkoa wowote nadhani hapa nchini, sasa kwa kawaida tembo wale hawawezi kwenda kwenye malisho wakiwa wamechanganyika na wanyama wengine wakiwa na ng'ombe na mbuzi," alisema.

Alitoa maelekezo kwa serikali kuchukua hatua kali dhidi ya wafugaji ambao wanavamia huko na hatimaye wanahatarisha wananchi wengine.

"Hasa kwenye hili tunafahamu kwamba athari zake zimekuwa kubwa, nataka nizishukuru jitihada za mkoa kwani wamejitahidi sana kuchukua hatua. Chama kinaielekeza serikali binadamu ni bora kuliko hao wanyama," alisema.

"Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na jitihada ambazo zimeelezwa zimeanza kuchukuliwa tunataka jambo hili, sasa watoke mstari wa mbele kuja kudhibiti na kuwarudisha nyuma hawa tembo wanaonekana kuzidi mitaani siku hadi siku hali sio nzuri.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Swissport, Mrisho Yassin (kushoto), akizungumza wakati wa kutangaza gawio kwa wanahisa wake katika mkutano mkuu jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TMA yatahadharisha upepo, kipupwe

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imetoa utabiri wa msimu wa Juni hadi Agosti ambao ni majira ya kipupwe huku baridi ya wastani na joto la kiasi vikitarajiwa katika maeneo mengi ya nchi.

Kwa mujibu wa utabiri huo uliotolewa jana, mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Tanga inatarajiwa kuwa na hali ya baridi ya wastani inayofikia nyuzi joto kati ya 18 na 26.

Maeneo ya Nyanda za Juu Kusini ya mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe, Songwe na baadhi ya maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro, yanatarajiwa kuwa na hali ya baridi inayofikia nyuzi joto nne mpaka 14.

Aidha, maeneo ya kaskazini ya nchi, mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara yanatarajiwa kuwa na nyuzi joto kati ya 10 na 18.

Utabiri huo unatanabahisha kwamba hali nyingine ya baridi inatarajiwa katika mkoa wa Ruvuma ambapo hali ya nyuzi joto inatarajiwa kufikia sita mpaka 14.

Pia mikoa ya Kanda ya Ziwa, Mwanza, Mara, Geita, Kagera, Shinyanga na Simiyu kiwango cha joto la chini kinatarajiwa kuwa cha kawaida hadi juu ya kawaida kufikia nyuzi joto 14 mpaka 20.

Mikoa ya Kanda ya Kati, Singida na Dodoma kinatarajiwa kuwa na baridi ya kawaida hadi joto kiasi kufikia nyuzijoto 12 mpaka 18. Pia mikoa ya Tabora, Rukwa, Katavi na Kigoma inatarajiwa kuwa na baridi kiasi hadi joto kiasi kufikia nyuzijoto 14 mpaka 20.

Akizungumza wakati wa kutoa utabiri huo, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Ladislaus Chang'a, alisema katika kipindi hiko cha kipupwe, magonjwa ya mifugo kama homa ya mapafu na hali ya vumbi na upepo yanatarajiwa kwa baadhi ya maeneo, hivyo wananchi wanapaswa kuchukua hatua.

"Ni kipindi ambacho kwa baadhi ya maeneo kunakuwa na mlipuko wa magonjwa kama ya macho hususani maeneo ya vumbi. Ni vyema hatua kuchukuliwa kukabiliana nayo," alisema Dk. Chang'a.

Alisema kwa ujumla duniani kuna mabadiliko makubwa ya hali ya joto na kinachotokea sasa chini ni sehemu ya mabadiliko hayo.

# Nape aonya huduma za simu bila ridhaa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Nape Nnauye, ameiagiza Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) pamoja na kampuni za simu kukomesha tabia ya kuunganisha wateja kwenye huduma wasizozihitaji.

Nape alitoa maagizo hayo jana jijini Dodoma alipopokea taarifa ya utekelezaji wa maagizo yake kwa kampuni za simu nchini iliyotolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Vodacom Tanzania.

Alisema kampuni za simu pamoja na TCRA wanapaswa kukaa pamoja na kutafuta njia ya pamoja kukomesha tabia ya wateja kuunganishwa na huduma ambazo hawazihitaji katika mitandao mbalimbali.

Maagizo yangu kwa kampuni za simu zote nchini na TCRA mtafute njia ambayo itasaidia kukomesha malalamiko ya wateja kuunganishwa na huduma wasizozihitaji na kuendelea kukatwa fedha hii tukomeshe mara moja," aliagiza.

Nape alisema siyo jambo la busara kampuni za simu kuendelea na tabia ya kuunganisha wateja katika huduma wasizozihitaji bila ridhaa yao.

Pia aliigiza TCRA pamoja na kampuni za simu kukaa pamoja na kutengeneza programu tumizi ambayo itatumika na wateja kusoma matumizi yao ya bando ili kuondoa malalamiko ambayo yamekuwa yakijitokeza.

"Matumizi ya bado yamekuwa yakilalamikiwa sana na wananchi, hivyo kampuni za simu pamoja na TCRA mtafute programu hiyo tumizi ambayo itamwezesha hata mwananchi wa chini kuwa na uwezo wa kusoma kiasi cha bando ambacho amekitumia ili kuondoa malalamiko," aliagiza.

Alisema kutokana na Watanzania wengi kutokuwa na uwezo wa kumiliki simu janja, TCRA na kampuni za simu zinapaswa kuja na utaratibu maalum wa kuwauzia wateja wao.

"Mnaweza hata kuja na utaratibu wa kuwakopesha simu, mnawapa na kulipa kidogo kidogo kwa utaratibu fulani kama ambavyo nchi zingine za wenzetu wanavyofanya, siyo lazima iwe pesa taslimu, hii itasaidia kuongeza matumizi ya intaneti nchini," alisema.

Mkurugenzi wa Masuala ya Kisekta TCRA, Dk. Emmanuel Manase, alisema lengo la serikali ni kuboresha huduma za mawasiliano nchini.

Dk. Manase alisema serikali ilitoa maagizo kwa kampuni za simu kufanyia kazi malalamiko ambayo imekuwa ikiyapokea kutoka kwa wananchi ili kuboresha utoaji huduma.

Mkurugenzi mtendaji wa Vodacom Tanzania, Sitholizwe Mdlalose, alisema wametekeleza maagizo yaliyotolewa na serikali kwa kuwatembelea wadau wao katika maeneo mbalimbali na kubaini kero zinazowakabili na kuzifanyia kazi.

"Katika maeneo tuliyokwenda tumebaini bado kuna changamoto ya upatikanaji wa mtandao hasa katika maeneo ya vijijini, hivyo tunakwenda kuwekeza nguvu katika kutatua kero hiyo.

"Kuna maeneo ambayo wateja wamependekeza kuwa mtandao wa 3G kwa sasa hauwatoshi, hivyo wanahitaji kuwekewa 5G na sisi hili tunalifanyia kazi,"

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kasi ya kuunganisha umeme iongezeke

**JANA** Wizara ya Nishati iliwasilisha bungeni makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2022/23, iliyojikita kuimarisha upatikanaji wa umeme kutoka kwenye vyanzo mbalimbali, upatikanaji na bei za mafuta. Bajeti hiyo imeonyesha vyanzo vipya ambavyo awali havikuwahi kutumika, huku kukiwa na mkataba na sekta binafsi zilizojikita kwenye uzalishaji wa nishati jadidifu.

Pia imelenga kusambaza gesi asilia kwenye makazi ya watu katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Kilimanjaro huku ikisafirishwa kwenda nchi za Kenya na Uganda baada ya kukamilisha makubaliano baina ya pande hizo.

Kwa Dar es Salaam vitajengwa vituo vya kugandisha gesi asilia, pia wataunganisha kwenye nyumba 670 za Sinza 225, Police Barracks Kurasini 345, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) 100 na kiwanda cha Raddy Fiber Manufacturing Tanzania Ltd cha Mkuranga.

Vyanzo vipya vya vitano vya nishati ni jotoardhi vya Ngozi na Kiejo - Mbaka mkoani Mbeya, Songwe, Luhoi Pwani na Natron Arusha, ambavyo baada ya upembuzi yakinifu ilibainika vitazalisha megawati 200.

Nyingine ni nishati ya jua na katika mwaka ujao wa fedha serikali itaanza ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa jua Shinyanga, utakaogharimu Euro milioni 115.30 (sawa na Sh. bilioni 286.2) na kwamba jumla ya Sh. bilioni 9.55 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme jua megawati 50 na kukamilisha taratibu za ufadhili wa awamu ya pili ya megawati 100.

Waziri wa Nishati, Januari Makamba, aliliambia Bunge kuwa kumekuwa na changamoto ya kukatika kwa umeme nchini kutokana na miundombinu ya kuzidiwa kutokana na kuongezeka kwa mahitaji kwa sasa, uchakavu wa miundombinu na shughuli za kibinadamu kama vile magari kugonga nguzo, nguzo kuchomwa moto na hujuma katika moto na hujuma. Alisema ili kuimarisha miundombinu ya usambazaji umeme, serikali imeendelea kutayarisha na kutekeleza miradi ya kusambaza nishati hiyo katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Dodoma na Pwani, itakayowezesha kuondokana na changamoto ya kukatika kwa umeme mara kwa mara ili kuwa na uhakika.

Mchanganuo wa uwezo wa mitambo ya kufua umeme katika gridi ya taifa kwa kila kimoja kiwango cha megawati kwenye mabano ni maji (574.60), gesi asilia (1,021.32) na tungamotaka (10.50) na kufanya jumla ya megawati 1,694.55.

Kwa mujibu wa waziri huyo, mahitaji ya juu ya umeme katika mfumo wa gridi ya taifa yameendelea kukua na kufikia Megawati 1,335.01 hadi Machi 25, mwaka huu saa 2:00 usiku, ikilinganishwa na megawati 1,201.02 zilizofikiwa mwaka 2020/21, ikiwa ni ongezeko la asilimia 11.16.

Tunaamini kupitia bajeti hii wananchi wataendelea kupata huduma ya umeme ipasavyo, kuanzia walioomba kuunganishiwa na kulipa na wanaotamani kufikiwa na huduma hiyo.


Ni muhimu nchi ikajipanga vyema kuendeleza vyanzo vya nishati jadidifu kwa kuwa ndiyo msukumo wa dunia, lakini kuendelea kushirikiana na sekta binafsi ili huduma iwafikie wananchi wengine na kwa haraka. Kuna viwanda vinazalisha umeme kutokana na mabaki ya miwa vinaliuzia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), lakini wapo wengine wanaweza kuzalisha umeme wa jua kwa ajili ya matumizi yao ni muhimu kuangalia.

Pia kumekuwa na malalamiko ya urasimu kwa wawekezaji binafsi ambao wamewekeza kwenye sekta hiyo kutokana na kuwapo vibali zaidi ya 30 wanavyotakiwa kuvifuata sehemu tofauti nchini, jambo linalowapa gharama kubwa.

Wakati tukiendelea na vyanzo vilivyozoeleka ni muhimu kuwekeza na kuwa makini na uwekezaji unaofanywa kwenye vyanzo vya nishati jadidifu ambavyo ni rafiki kwa mazingira ambavyo ni jua, upepo, mawimbi na upepo wa bahari na tungamotaka, ili inapofika ulazima wa kuachana na gesi, mafuta na maji kuwe na maandalizi ya kutosha.

Maji ni chanzo kizuri cha kuzalisha umeme, lakini kutokana na mabadiliko ya tabianchi inapotokea ukame vyanzo hukauka na kushindwa kuzalisha nishati hiyo, mara kadhaa Tanzania imepitia mgawo sababu ikiwa ni kukauka kwa mabwawa ya kuzalisha nishati hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tunachukua hatua zipi kukabili sumu kutoka vipisi vya sigara?

Na Yasmine Protace

**NI** kawaida katika mazingira nchini, jamii imekuwa na kawaida kuona vipisi vya sigara vinavyotupwa kwenye maji au barabarani, hatujui madhara yake kwa afya za umma.

Tunaviona vipisi vya sigara vikiwa maeneo mbalimbali vimetupwa, lakini madhara yake hayajulikani kwa kina.

Kinachotakiwa sasa ni elimu hiyo iendelee kutolewa kwa watumiaji sigara pale wanapomaliza kutumia sigara zao, pia usahihi wa mahali pa kuhifadhi.

Hata kuhamia penye matumizi ya uvutaji holela wa sigara, napo kuna changamoto za kiafya kwa wanaouvuta moshi wa sigara hizo.

Wapo watu wenye tabia, wanavuta sigara katika kwenye kumbi za starehe, katika magari na majumbani. Kwa kufanya hivyo, ni hali inayowaathiri kiafya wote wanaoingiwa na moshi huo wa tumbaku.

Sigara imedumu kihistoria ni moja ya starehe, ambayo anayetumia anafurahi kwa kila anachokipata kupitia sigara hiyo.

Hata hivyo, inaelezwa kwamba vishungi vyake ni kati ya vitu vyenye uchafuzi na sumu kubwa inayopatikana katika vyanzo vya maji.

Katika hilo nina la kumrejea Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, kwenye viwanja vya Bunge jijini Dodoma, wakati akitoa tamko kwenye maadhimisho ya Siku ya Kutotumia Tumbaku Duniani yenye kaulimbiu "Tumbaku: Tishio la Mazingira Yetu".

Waziri Ummy anasema kwamba, inamchukua muda mrefu kwa kitako cha sigara kuoza, hivyo kuruhusu nikotini na kemikali kuingia kwenye mifumo ya ikolojia inayozunguka, inayoathiri maisha ya binadamu. "Tafiti zinaonyesha kwamba vishungi vya sigara vinapowekwa kwenye maji, vinaweza kutoa kemikali ambazo huweza kusababisha vifo vya viumbe wa majini, wakiwamo samaki," anatamka waziri huyo mwenye dhamana.

Pia, ana la kuongozea kuwa ni takribani asilimia 65 ya wavutaji hutupa vishungi vya sigara barabarani, kwenye fukwe baharini, pia ziwani.

Vilevile, inatajwa plastiki zinazohusiana na sigara za kielektroniki ambazo zaidi ziko katika mataifa yaliyopiga hatua, huishia kutupwa kwenye mifereji ya maji na barabarani, hivyo kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira.

Nini kifanyike? Waziri Ummy ambaye kitaaluma ni mwanasheria, ametoa miezi miwili kwa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TMDA), akitaka ifanye utafiti wa shisha kuwekwa dawa za kulevya kwa kushirikiana na Tume ya Dawa za Kulevya nchini.

"Maelekezo yangu ni kufanya tathmini ya bidhaa hizi ili kulinda afya za jamii, kwani kufanya biashara ya shisha ujue unafanya kosa la jinai, Sheria ya Kudhibiti Matumizi ya Bidhaa ya Tumbaku nchini Sura ya 121 haijatekelezwa kikamilifu, TMDA mfanye tathmini kwa kina," akasema.

Pia Waziri Ummy anasema magonjwa mengi yasiyo ya kuambukiza, yamekuwa yakiongezeka kila siku, yakileta maradhi mbalimbali yanayosababishwa na matumizi holela ya bidhaa za tumbaku.

"Jamii inatakiwa kupunguza au kuacha kabisa matumizi ya tumbaku au bidhaa zake kwa ajili ya afya zetu, kwani wanaotumia bidhaa ya tumbaku zaidi ya asilimia 50 wanafariki," anasema.

Kwa sasa nchini, kuna takribani vifo 14,700 kila mwaka vinavyotokana na matumizi ya tumbaku na asilimia 8.7 ya Watanzania sawa na milioni 2.6 wanatajwa kutumia tumbaku.

Anasema wengi huathirika na moshi wa sigara katika maeneo ya kazi, kwenye baa, kumbi za starehe na migahawa na utafiti umeonyesha asilimia 77 ya watu hao huvutishwa sigara kwenye baa, asilimia 31.1 kwenye migahawa na asilimia 13.8 majumbani.

Takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), zinaeleza bidhaa tumbaku husababisha vifo kwa takribana nusu ya watumiaji wake na zaidi ya watu takribani milioni nane hufa kila mwaka duniani kwa sababu ya kutumia tumbaku.

Anaeleza, jumla ya watu milioni saba ni zao la vifo vya matumizi ya moja kwa moja, wakati wengine milioni 1.2 wanatokana na utumiaji bidhaa za tumbaku usio wa moja kwa moja.

# NEMC yaonya hospitali, vituo vya afya majitaka

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BARAZA la Taifa la Hifadhi ya Mazingira (NEMC) limezitaka hospitali kubwa na vituo vya afya vinavyohudumia watu wengi, kutibu majitaka kabla ya kuruhusu kutiririka kwenye mazingira.

Meneja wa Baraza Kanda ya Kati, Dk. Franklin Rwezimula, aliyasema hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari kuelekea kilele cha Siku ya Mazingira Duniani itakayofanyika kitaifa jijini Dodoma.

"Nitoe rai kwa hospitali na vituo vya afya kuhakikisha majitaka yanayotokana na kazi za hospitali, wawe na mifumo ya kuyatibu na baada ya kutibiwa, ndiyo yaruhusiwe kuingia kwenye mazingira," alisema.

Aliwataka wawe na utaratibu wa kutenganisha taka ili kurahisisha kuziteketeza, hospitali ziwe na vichoma moto na zizingatie matumizi ya nishati ambayo ni rafiki wa mazingira.

"Baadhi ya watu wanatumia kuni lakini sisi tunataka watu watumie gesi ambayo ni rafiki wa mazingira kama Benjamin Mkapa, wanatumia gesi," alisema.

Alipongeza Hospitali ya Benjamin Mkapa kwa kuzingatia masuala ya mazingira kwa kuwa na mfumo wa kutibu majitaka.

"Vitu ambavyo tulitaka Benjamin Mkapa wazingatie juzi tulipokwenda wamezingatia, wana mfumo wa kutibu majitaka, wana kichoma taka cha kisasa," alisema.

Pamoja na hayo, aliwahimiza wananchi kuacha kukata miti ovyo kwa kuwa wanaharibu mazingira na wanasababisha kukumbwa na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Pia aliwashauri wanafunzi wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini (IRDP) kujiunga kwenye programu ya wataalamu elekezi ambapo watajiajiri wenyewe na kufanya shughuli za maandiko na tathmini ya mazingira.

Alisema kwa sasa Tanzania inakabiliwa na uhaba wa wataalamu wa kuandika tathmini ya mazingira na kwamba wanaamini chuo hicho kitatoa wataalamu wengi watakaosaidia kupunguza pengo lililoko la wataalamu hao nchini.



Wananchi wa Kijiji cha Nyabihanga, Kata ya Bukiliro, wilayani Ngara, mkoani Kagera, wakipatiwa mafunzo ya Sheria ya Mazingira na Ardhi yaliyofadhiliwa na Kampuni ya Tembo Nickel hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi waonywa kuharibu vyanzo maji

**Na Mwandishi Wetu,** NGARA

WANANCHI wilayani Ngara mkoani Kagera wamepewa mafunzo ya sheria ya ardhi na mazingira huku wakitakiwa kuacha kuuza ardhi kiholela na kuacha kulima kwenye vyanzo vya maji.

Elimu hiyo inatolewa na maofisa wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara kwa kufadhiliwa na Kampuni ya Tembo Nickel.

Maofisa hao walitoa elimu hiyo jana katika vijiji vya Mumilamila, Nyabihanga, Bugarama, Mukubu Rwinyana na Muganza.

Cosmas Lubambura, ambaye ni Ofisa Ardhi Wilaya ya Ngara, akitoa elimu hiyo kwa nyakati tofauti, aliwataka wananchi hao kuacha tabia ya kuuza ardhi bila kufuata sheria.

"Wakati mwingine mmekuwa mkiuza ardhi hata kwa wananchi wa nchi jirani, jambo ambalo ni kinyume cha sheria," alisema.

Pia aliwataka kuhakikisha wanafuata sheria pale wanapolazimika kuuza ardhi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha mashahidi wanakuwa majirani na kwa walioa washirikishe wake zao ili kuepuka migogoro.

Ofisa Atanasio Andrew ambaye ni ofisa mazingira wa halmashauri hiyo, aliwataka wananchi hao kuacha tabia ya kulima kwenye vyanzo vya maji, akisema shughuli za binadamu kwenye vyanzo vya maji zimeanza kupunguza wingi wa maji katika maeneo hayo.

Alisema baadhi ya wananchi wa wilaya hiyo pia wamekuwa na tabia ya kuchoma moto ovyo, jambo ambalo ni hatari kwa kuwa wakati mwingine huathiri mazao ya watu wengine.

"Inatakiwa mtunze mazingira ili mpate faida ya fursa mbalimbali, wenzetu (Tembo Nickel) wanatambua na kuthamini mchango wa mazingira na ndiyo maana wameamua kudhamini mafunzo haya.

"Shughuli za mgodi zikianza kweli mazingira yanaweza kuathiriwa kwa kiasi fulani, lakini mpango wa kudhibiti madhara ya mazingira ulioandaliwa na mgodi na kupitishwa na serikali utafuatwa kuhahikisha madhara yanapungua au kumalizwa kabisa," alisema.

Basil Shio kutoka kampuni ya RSK ambayo imepewa kandarasi ya kufanya tathmini na kuhamisha watu na makazi ili kupisha mradi wa Tembo Nickel wakati ukifika, alisema jukumu lao ni kujua shughuli za kiuchumi, kukagua mali, kufanya tathmini na kwa wananchi ambao nyumba zao zipo kwenye eneo la mradi watahamishiwa maeneo mbadala.

"Tutapita kuchukua taarifa za watu, ukubwa wa maeneo kwa mtu mmoja mmoja na kuandaa majedwali ya malipo kwa mujibu wa sheria, kisha uhamishaji watu na wakazi utafuata.

"Tutakaa sana na ninyi viongozi na pia wananchi wanaoguswa na mradi, wote tutakaa nao, tuongee na kujibu yote mliyonayo," alisema.

Mafunzo hayo yalipokewa vizuri na wananchi pamoja na Mkuu wa Wilaya ambaye alishasisitiza kwamba wananchi wasidanganywe na kurubuniwa na watu wa nje ambao wanataka ardhi kwa udanganyifu kutoka kwa wakazi na kuwanyima haki zao wakati wa operesheni ondoa tengesha Ngara.

## CEOrt yapata kiongozi mpya

**Na Gwamaka Alipipi**

JUKWAA la Maofisa Watendaji Wakuu (CEOrt) limempitisha David Tarimo kuwa Mwenyekiti wa Bodi wa Jukwaa hilo, akichukua nafasi ya Sanjay Rughani.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa CEOrt, Santina Benson, uteuzi wa Tarimo ulianza juzi.

Santina alisema Rughani alikuwa Mwenyekiti wa Bodi ya CEOrt tangu mwaka 2018 na alikuwa kiongozi wa pili kushika nafasi hiyo tangu jukwaa hilo liliposajiliwa rasmi. Wa kwanza akiwa ni Ali Mufuruki.

Alisema katika kipindi chote cha uongozi wake, Rughani alionyesha uongozi bora na kusaidia kuongoza shirika katika kipindi cha ukuaji mkubwa.

Santina alisema wakati wa uongozi wake, Rughani alichukua jukumu muhimu katika kuzindua programu mbalimbali, mpango wa uongozi bora na juhudi za kitaifa za kujenga uwezo wa wakurugenzi wakuu wenye maono kwa ajili ya siku zijazo.

"Rughani alikuwa mstari wa mbele kuhamasisha utekelezaji endelevu wa biashara, akiongoza kwa mfano na mara nyingi kuzungumza juu ya jukumu la sekta binafsi.

Pia ilishuhudia ukuaji wa wanachama ukilinganisha na hapo awali ikiwa ni ongezeko la wanachama wapya zaidi ya asilimia 40," alisema Santina.

Alisema Rughani ametetea miradi kadhaa yenye matokeo chanya ya kijamii na kiuchumi kutoka katika kukuza uwakilishi wa wanawake katika uongozi hadi kuongoza juhudi za ushirikiano na serikali kwa madhumuni ya pamoja ya ustawi wa Tanzania.

Santina alisema: "CEOrt inachukua fursa hii kumkaribisha David Tarimo. Uzoefu wake ni pamoja na masuala ya sera za kodi kwa kampuni zinazofanya kazi nchini na katika sekta mbalimbali, lakini kwa kuzingatia hasa madini, mafuta na gesi na huduma za muhimu."

HABARI KITAIFA

# SBL yageukia usawa kwa makundi ya jamii

**Na Frank Monyo**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) imesema itaendelea kutoa kipaumbele pamoja mchango wake katika kusaidia shughuli mbalimbali za kimaendeleo na kuhamasisha usawa kwa makundi yote katika jamii.

Mkakati wa SBL unakwenda sambamba na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Serikali 2021/22-2025/26 unaotaja baadhi ya vipaumbele ambavyo baadhi SBL imekuwa ikivitekeleza kupitia miradi yake ya kusaidia jamii.

Jijini Dar es Salaam juzi, Mkurugenzi wa Uhusiano kwa Umma wa SBL, John Wanyancha, alisema kampuni hiyo kupitia mpango wake wa 'Mama Diageo', imeweka malengo ya kuleta matokea chanya katika kusaidia jamii ambayo yanajulikana kama Society 2030.

Alisema kuwa kupitia mpango huo wa miaka 10, SBL imekuwa ikitekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kama vile kusaidia wakulima, kusaidia upatikanaji wa majisafi na salama, kufadhili wanafunzi, kuhamasisha usawa kwa makundi yote na kutilia mkazo uwezeshaji wanawake.

"Kwa mfano, tunayo programu ya kuwafadhili wanafunzi wa kilimo ambao wana uwezo mzuri darasani na ambao wanatoka katika familia zenye kipato duni. Katika programu hii ambayo inalipa gharama zote za masomo kwa wanufaika, tunahakikisha nusu yao ni wanawake," alisema.

Katika mrengo huo huo wa kuwawezesha wanawake, Wanyancha alisema SBL inaendesha programu ya STEM ambayo huchukua wanafunzi wa kike wanaosoma masomo ya sayansi na waliofanya vizuri, wakipewa fursa ya kujiunga na SBL na kujifunza kwa vitendo kwa kipindi cha mwaka mzima.

"Kwenye maendeleo ya jamii tumesaidia upatikanaji wa majisafi na salama kwa kufadhili uchimbaji wa visima. Tangu mwaka 2010, tumechimba visima 18 katika sehemu mbalimbali nchini na kuwezesha upatikanaji wa huduma hii muhimu kwa watu zaidi ya milioni mbili," alifafanua.

Mkurugenzi huyo alisema SBL inafanya kazi na mtandao wa wakulima zaidi ya 400 nchini na huwawezesha kwa kuwapa mbegu bila malipo, huduma za ugani na kuwaunganisha na benki kwa ajili ya kupata mikopo huku ikiwahakikishia masoko kwa mazao yao ambayo hutumika kutengenezea bia.



Meneja Mkuu wa hoteli ya nyota tano ya Johari Rotana, Joerg Potreck, akizungumza na waandishi wa habari, wakati wa ufunguzi wa hoteli hiyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TADB yaangazia uwezeshaji vijana, wanawake kilimo

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imeandaa mkakati wa kuwawezesha kiuchumi wanawake na vijana kwa kushirikiana na kituo cha uwezeshaji katika Uwezeshaji- Investment Climate Reform Facility (ICR).

Taarifa iliyotolewa jana na benki hiyo ilisema mkakati huo umeanza kwa warsha ya mashauriano baina ya TADB na ICR ili kujadili namna ya kuwainua wanawake na vijana katika kilimo. "Juhudi za TADB zinalenga kwa makusudi katika kuziba pengo la kiuchumi kati ya wanawake na vijana kwani takwimu za Finscope zinaonyesha kuwa makundi hayo ni asilimia 50 ya nguvu kazi lakini hayajajumuishwa katika sekta rasmi ya fedha na asilimia sita tu ya wanawake hawana akaunti za benki huku asilimia 26 pekee ya vijana wakiwa wakulima," ilisema taarifa hiyo.

"TADB imeandaa warsha hiyo ili kupata utaalamu zaidi wa kiufundi kutoka ICR chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya. Mpango huu unalenga kuifahamisha TADB na taasisi zingine za fedha kuhusu hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kuongeza ushirikishwaji wa kifedha miongoni mwa wanawake na vijana katika sekta ya kilimo," iliongeza taarifa.

Warsha hiyo ya siku mbili imejumuisha wawakilishi kutoka wizara mbalimbali za Muungano na Zanzibar, ujumbe wa Umoja wa Ulaya nchini Tanzania na mashirika ya wanawake na vijana. Washiriki walipata fursa ya kujadili maoni yao kuhusu bidhaa na huduma za kilimo kwa wanawake na vijana.

Aidha, washiriki walikubaliana kuwa mpango unapaswa kujumuisha aina mbalimbali za bidhaa za kifedha kama vile utaratibu wa udhamini, utoaji wa mikopo ya moja kwa moja, na njia za mikopo kwa taasisi za fedha washirika.

Mpango huo pia utajumuisha ushirikiano kati ya TADB na wawezeshaji wa soko ili kutoa taarifa za soko, mafunzo, na kukuza uwezo kwa wakulima wachanga na wanawake.

# Hoteli iliyofungwa miaka 2 yaanza kutoa huduma

**Na John Badi**

HOTELI ya nyota tano ya Johari Rotana imeanza kutoa huduma baada ya kufungwa kwa miaka miwili kutokana na athari za UVIKO-19.

Kutokana na kuondolewa kwa vikwazo vya usafiri, idadi ya watalii wa kimataifa wanaowasili Tanzania imekuwa ikiongezeka hali ambayo imechangia ushawishi chanya na ukuaji katika sekta hiyo inayohudumia wageni.

Joerg Potreck, Meneja Mkuu wa Johari Rotana, alisema jana kuwa: "Ufunguzi wetu umekuja wakati mwafaka baada ya Tanzania kutajwa kuwa nchi inayoongoza kwa kutembelewa na watalii yaani 'Africa's Leading Destination' kwa mwaka 2021 na utitiri wa watalii nchini. Ni jambo la furaha kwetu wote na timu yangu imejipanga kuwakaribisha wageni wetu tena hapa Johari Rotana."

Alisema hoteli hiyo inapatikana kwa urahisi katika eneo la MNF Square katika mkoa wa kibiashara wa Dar es Salaam.

"Hii imeweka viwango vipya katika usanifu, muundo, teknolojia na ubora wa huduma, katika hoteli yetu ya Johari Rotana, ambayo ni hoteli yetu ya kwanza kwenye Kanda ya Afrika Mashariki, imejizatiti kufanya mapinduzi makubwa katika sekta ya ukarimu.

"Tuna uhakika kwamba vyumba vyetu vya kulala, kumbi za vyakula na vinywaji, vifaa vya hali ya juu vya mikutano ikiwa ni pamoja na ukumbi mkubwa zaidi wa burudani nchini Tanzania, yaani ballroom na huduma nyingine vitavutia wageni wetu na kuleta ushindani wenye tija sokoni," alisema Potreck.

Alisema hoteli hiyo pia ina vyumba sita vya ziada vya mikutano na eneo la maji tiririka la kuvutia, yaani water front, kituo cha biashara, ofisi daraja A, na kituo cha maegesho ya ndani, na kuifanya kuwa chaguo bora kwa wageni wa biashara na burudani.

Baada ya kuzindua filamu ya Tanzania The Royal Tour jijini Arusha hivi karibuni, Rais Samia Suluhu alihimiza uwekezaji zaidi kwenye hoteli ili kuwapokea wageni wanaotarajiwa kutua nchini kutokana na hamasa iliyochagizwa na filamu hiyo.

## TANGAZO



Jamhuri ya Muungano
wa Tanzania

# Wizara ya Nishati

# Bajeti Ya Mwaka 2022/23

## Vipaumbele vya Bajeti

1. Kutekeleza miradi mbalimbali ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme, ikiwemo kupeleka umeme wa Gridi ya Taifa kwenye mikoa ya Katavi, Kigoma and Kagera na mradi mkubwa wa Kuimarisha Gridi ya Taifa (National Grid Stabilization Project).
2. Kutekeleza Miradi ya Nishati Vijijini pamoja na kuanza utaratibu wa kupeleka umeme katika Vitongoji vyote nchini.
3. Kukamilisha mazungumzo ya mradi wa LNG Lindi na kuanza maandalizi ya utekelezaji wake.
4. Kutekeleza miradi ya nishati jadidifu ikiwemo jotoardhi, tungamotaka, upepo na jua pamoja na matumizi bora ya Nishati (Energy Efficiency and Conservation).
5. Kuhakikisha upatikanaji wa mafuta ya kutosha nchini, ikiwemo uanzishwaji wa Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta (Strategic Petroleum Reserve) na Mfuko wa Kudhibiti Mabadiliko ya Bei za Mafuta (Fuel Price Stabilization Fund - FPSF).
6. Kuiimarisha TPDC na Kampuni zake Tanzu za TANOIL na GASCO.
7. Kuboresha miundombinu ya kupokea, kushusha, kuhifadhi na kutoa mafuta katika Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara na Ghala za dhamana ya forodha (Customs Bonded Warehouse) na Kituo cha Pamoja cha kupokelea Mafuta kutoka Melini (Single Receiving Terminal).
8. Kuimarisha utendaji wa taasisi za Wizara, hasa TANESCO, EWURA na PBPA, na huduma zinazotelewa na taasisi hizo.
9. Kuongeza ushiriki na uwekezaji wa Sekta Binafsi katika sekta ya Nishati.
10. Kuhakikisha ushiriki wa wazawa katika shughuli za mafuta na gesi asilia unaimarika.
11. Kufufua Shughuli za utafiti na utafutaji wa mafuta na gesi asilia.
12. Kuongeza matumizi ya nishati ya gesi kwa kupikia (LPG) na kwenye magari na viwandani (CNG).

# TANGAZO


## Miradi Ya Kuzalisha Umeme Iliyopo Katika Hatua Za Utekelezaji

| MIRADI | THAMANI YA MRADI | FEDHA ZILIZO TENGEWA 22/23 (Shilingi) |
|---|---|---|
| Mradi wa kuzalisha Umeme kwa kutumia maji wa Julius Nyerere Hydro Power project (JHNIPP) -MW 2,115 | Shilingi Trilioni 6.55 | Trilioni 1.44 |
| Mradi wa kuzalisha Umeme kwa kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi 1 Extension - MW 185 | Dola za Marekani milioni 188 | Bilioni 35 |
| Mradi wa kuzalisha Umeme kwa kutumia Maji wa Rusumo - MW80 | Dola za Marekani milioni 113 | Bilioni 9.94 *(Fedha za Nje)* |

## Miradi Ya Kuzalisha Umeme Iliyopo Katika Hatua Za Utayarishaji

| MIRADI | THAMANI YA MRADI | FEDHA ZILIZO-TENGEWA 22/23 (Shilingi) |
|---|---|---|
| Mradi wa kuzalisha Umeme kwa kutumia Maji wa Ruhudji - MW 358 (conceptual design) | Dola za Marekani milioni 407.4 | Bilioni 15.0 |
| Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa kutumia Maji wa Kakono - MW- 87 | Dola za Marekani milioni 287.6 | Milioni 150 |
| Mradi wa kuzalisha Umeme kwa kutumia Maji wa Rumakali - MW 222 (conceptual design) | Dola za Marekani milioni 388.22 | *Bilioni 8.0* |
| Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa kutumia Maji wa Malagarasi - MW 49.5 | Dola za Marekani milioni 144.14 | *Bilioni 13.97 (fedha za nje)* |
| Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa kutumia Maji wa Kikonge - MW 300 | Dola za Marekani milioni 795.4 | *Bilioni 1.45* |
| Mradi wa kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Mtwara - MW 300 | Dola za Marekani milioni 421.1 | *Milioni 600* |
| Mradi wa kuzalisha Umeme Jua wa Shinyanga - MW 150 | Euro Milioni 115.30 | *Bilioni 9.55 (fedha za nje)* |
| Ukarabati wa Mitambo katika kituo cha Kuzalisha Umeme cha Hale | | *Bilioni 10.25 (fedha za nje)* |

## Mtandao wa Njia za Kusafirisha Umeme Nchini (National Grid Network) hadi kufikia mwezi Mei, 2022




## Miradi Ya Kusafirisha Na Kusambaza Umeme Iliyopo Katika Hatua Za Utekelezaji

| MIRADI | THAMANI YA MRADI | FEDHA ZILIZO-TENGEWA 22/23 (Shilingi) |
|---|---|---|
| Julius Nyerere Hydro Power Plant hadi Chalinze - kV 400 | Dola za Marekani milioni 51.4 na Shilingi bilioni 31.9 | Bilioni 180.00 |
| Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Singida- Arusha - Namanga | Dola za Marekani milioni 258.82 | Bilioni 7.65 (fedha za nje) |
| Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 220 ya Geita - Nyakanazi | Euro milioni 45 | *Bilioni 6.53 (fedha za nje)* |
| Mradi wa Njia ya Kusafirishia Umeme Msongo wa kV 220 Rusumo - Nyakanazi | | *Bilioni 3.30* |
| Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma | Dola za Marekani milioni 35 | *Bilioni 7.14 (fedha za nje)* |
| Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Iringa- Mbeya - Tunduma hadi Sumbawanga | Dola za Marekani milioni 595 | *Bilioni 34.71 (fedha za ndani na za nje)* |
| Ujenzi wa Njia ya Kusafirishia Umeme Msongo wa kV 220 kwaajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme (Standard Gauge Railway - SGR) | | Mradi huu utekelezwa kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi |
| Mradi wa Ukarabati na Uboreshaji wa Gridi ya Taifa (Grid Rehabilitation and Upgrading) | | Sehemu ya Mradi huu umefadhiliwa na AFD, Serikali imetenga Bilioni 8.43 (fedha za nje) |

## Miradi Ya Kusafirisha Na Kusambaza Umeme Iliyopo Katika Hatua Za Utayarishaji

| MIRADI | THAMANI YA MRADI | FEDHA ZILIZO-TENGEWA 22/23 (Shilingi) |
|---|---|---|
| Chalinze- Kinyerezi kV400 | Kwa upande wa Njia ya kusafirisha Umeme Dola za Marekani Milioni 42.882, na Kituo cha cupola Umeme Dola za Marekani milioni 71.4 | Bilioni 40.00 |
| Chalinze- Dodoma na Chalinze - Segera kV 400 | Dola za Marekani milioni 285.02 | Milioni 225.00 |
| Chalinze- Bagamoyo na Segera Tanga kV 220 | Dola za Marekani milioni 163.21 | *Milioni 50.00* |

## TANGAZO

| | | |
|---|---|---|
| Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Sumbawanga hadi Kigoma kupitia Mpanda na Kituo cha Kupoza Umeme Mpanda | Dola za Marekani milioni 200.4 Kwa upande wa Njia ya kusafirishia Umeme na Dola za Marekani milioni 59 kwa Kituo cha kupoza Umeme. | |
| Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Somanga Fungu hadi Mkuranga | Dola za Marekani milioni 150 | *Bilioni 4.85* |
| Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 na Kituo cha Kupoza Umeme Katika Mkoa wa Simiyu | Shilingi bilioni 75 | *Milioni 725.00* |
| Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Benaco hadi Kyaka na Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Benaco na Upanuzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Kyaka. | Dola za Marekani milioni 119.4 | |
| Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 132 kutoka Urambo mkoani Tabora hadi Kidahwe mkoani Kigoma | Shilingi bilioni 69.7 | Bilioni 2.08 |
| Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 132 kutoka Tabora hadi Katavi kupitia Ipole na Inyonga | Shilingi bilioni 69.7 | Bilioni 5.08 |
| Mradi wa Kuboresha Mfumo wa Usambazaji Umeme Jiji la Dodoma | Dola za Marekani milioni 167.7 | Bilioni 6.57 |
| Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa (National Grid Stabilization Projects) | Shilingi trilioni 4.420 | Bilioni 400.00 |

### **Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa** (National Grid Stabilization Projects) **kwa Mwaka 2022/23 - Fedha zilizotengwa Billion 500.**

| Maeneo ya Utekelezaji |
|---|
| Kununua na kufunga mashineumba (transformers) 6,000 |
| Kununua na kusimika nguzo za njia za kusafirisha umeme 380,000 |
| Kununua na kufunga nyaya zenye urefu wa Kilomita 46,200 |
| Kununua na kufunga Mita za Luku 700,000 |
| Kujenga vituo vya kupooza umeme (grid substations) 14 za 220/33kv na 132/33kv |
| Kununua na kufunga mashineumba kubwa (power transformers) 27 za size ya 50MVA, 60MVA, 90MVA na 120MVA |
| Kujenga njia za kusafirisha umeme za urefu wa Kilomita 948 za msongo wa kV 132 na kV 220 |

## Miradi ya Umeme ya Sekta Binafsi iliyopo katika hatua mbalimbali (MW 3,443.62)

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Zuzu Project | Somanga Fungu Gas fired Project | Mradi mdogo wa maji Suma | Mradi mdogo wa maji Suma | Mradi mdogo wa maji TULILA | Mradi mdogo wa umeme jua Lumuma | Mradi mdogo wa maji Suma |
| Manyoni | Kibo Mining - Mbeya | Mradi mdogo wa maji Ilundo | Mradi mdogo wa maji Ilundo | Mradi mdogo wa maji DARAKUTA | Mradi mdogo wa umeme jua Kongwa | Mradi mdogo wa maji Luengere |
| Singida (Ikungi) Wind Project | Mapembasi - Njombe | Mradi mdogo wa maji Kiwira | Mradi mdogo wa maji Kiwira | Mradi mdogo wa maji YOVI | Mradi mdogo wa umeme jua Igunga | Mradi mdogo wa maji Idete |
| Makambako Solar Project | Somangafungu (KECL) | Mradi mdogo wa maji Luswisi | Mradi mdogo wa maji Luswisi | Mradi mdogo wa maji Madope | Mradi mdogo wa umeme jua Isangawana | Mradi mdogo wa umeme jua Convivium |
| Same Solar Project | Geo Wind - Singida | Mradi mdogo wa maji Igola | Mradi mdogo wa maji Igola | Mradi mdogo wa maji Maguta | Mradi mdogo wa umeme jua Gua | Mradi mdogo wa maji Kikuletwa II |
| Ngozi Geothermal Project | Mpanga (Iringa) | Mradi mdogo wa maji Lwega | Mradi mdogo wa maji Lwega | Mradi mdogo wa maji Ijangala | Mradi mdogo wa umeme jua Mbarali | Mradi mdogo wa maji Chimala |
| Mnyera Hydropower Project | Rukwa Coal (Edenville) | Mradi mdogo wa maji Nkwilo | Mradi mdogo wa maji Nkwilo | Mradi mdogo wa umeme jua Kahama | Mradi mdogo wa umeme jua Sumbawanga | Mradi mdogo wa maji Kamwana |
| Total Energies Solar Project | Mchuchuma - Njombe | Mradi mdogo wa maji Ifumbo | Mradi mdogo wa maji Ifumbo | Mradi mdogo wa maji Diwale | Mradi mdogo wa umeme jua Mpanda | Mradi mdogo wa umeme jua Bugando |
| | | Mradi mdogo wa maji Nakatuta | Mradi mdogo wa maji Nakatuta | Mradi mdogo wa maji Pinyinyi | | |

# TANGAZO

## Miradi ya kusambaza umeme vijijini

| MIRADI | THAMANI YA MRADI | FEDHA ZILIZO-TENGEWA 22/23 (Shilingi) |
| --- | --- | --- |
| Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili | Shilingi bilioni 1,240 | Bilioni 164.54 |
| Mradi wa Kusambaza Umeme Katika Vitongoji -(Hamlet Electrification Project - HEP) | Shilingi trilioni 6.5 | Bilioni 40.00 (kwa ajili ya maandalizi) |
| Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa 2B | Shilingi bilioni 227 | *Bilioni 14.08 ni mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya Ufaransa kupitia Shirika lake la AFD na Billioni 10.00 kutoka Serikali ya Tanzania* |
| Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa 2C | Shilingi bilioni 100 | *Bilioni 14.81 kutoka Serikali ya Norway na Billioni 16.29 Kutoka Serikali ya Tanzania* |
| Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme Ifakara (220/33kV, 1X 20MVA) na Ujenzi wa Miundombinu ya Usambazaji Umeme. | Shilingi bilioni 23.62 | *Bilioni 2.00 zimetengwa Katika kukamilisha mradi* |
| Mradi wa Kusambaza Umeme Maeneo ya Vijiji - Miji Awamu ya Pili (Peri- Urban) | | *Bilioni 31.33* |
| Mradi wa Kufunga Mfumo wa Umeme Jua Katika Taasisi za Umma Katina Wilaya Nane (Sustainable Solar Market Packages Phase II- SSMP) | | *Bilioni 1.50* |
| Mradi wa Kupeleka Umeme Kwenye Vijiji Katika Visiwa na Maeneo yaliyo mbali na Gridi ya Taifa | Shilingi bilioni 54.48 | *Bilioni 20.00* |
| Mradi wa kuwezesha Upatikanaji wa Nishati Bora ya Kupikia vijijini - Support Clean energy for cooking in Rural Areas | | *Billioni 10.00 kusambaza gesi asilia Katika makazi ya Wananchi walio katika mkuza wa bomba kuu la gesi Mikoa ya Mtwara, Lindi na Pwani* |
| Kampeni kubwa ya kuhamasisha matumizi na tafiti za Nishati bora ya kupikia | | *Milioni 500* |
| Mradi wa Kuwezesha Ujenzi wa Vituo Vidogo vya kusambaza Bidhaa za Petroli vijijini kwa Njia ya Mkopo Nafuu - Credit Line Facility | | *Bilioni 2.00* |
| Mpango wa Kuimarisha Vyanzo via Mapato ya Kugharamia Miradi ya Nishati Vijijini. | | *Milioni 500.00* |
| Mradi wa kuwezesha waendelezaji binafsi wa Miradi ya Nishati Katika mane ambayo haijafikiwa na Gridi ya Taifa | | *Bilioni 5.00* |
| Mradi wa kupeleka Umeme Katika Vituo vya Afya na Pampu za Maji ili Kuzuia Magonjwa ya Kuambukiza na UVIKO-19 | Shilingi bilioni 34.50 | *Bilioni 15.61 Kutoka Umoja wa Ulaya* |
| Mradi wa Kupeleka Umeme katika Maeneo ya wachimbaji wadogo wa Madini, Viwanda na Kilimo | Shilingi bilioni 100 | *Bilioni 20.00* |
| Mradi wa kupeleka Umeme katika Miradi ya Shule Vijijini pamoja na Mahakama za Mwanzo | | *Bilioni 10.00* |



Picha ya Saluni- Kinyozi Kijini

## Uendelezaji wa Rasilimali ya Joto Ardhi

| MIRADI | FEDHA ZILIZOTENGWA 22/23 (Shilingi) |
| --- | --- |
| Mradi wa Joto Ardhi Ngozi (Mbeya) - MW70 - programu ya uchorongaji wa visima vitatu cya uhakiki (exploratory wells) | Milioni 779.4 zimetengwa ambapo milioni 300 fedha za ndani na milioni 479.4 fedha za Nje. |
| Mradi wa Joto ardhi Songwe MW 5- kukamilisha uchorongaji wa visima vifupi (shallow wells) | Milioni 500 |
| Mradi wa Jotoardhi Kiejo- Mbaka (Mbeya) - MW 60 - uchorongaji na kutekeleza miradi ya matumizi mengine (direct heat uses) | Bilioni 2.89 |
| Mradi wa Joto Ardhi Natron (Arusha) MW 60 (Detailed surface exploration) | Bilioni 1.49 zimetengwa, kati ya hizo milioni 472.16 fedha za ndani na bilioni 1.02 fedha za nje. |

## Ramani ya Maeneo Mbalimbali yenye Viashiria vya Uwepo wa Rasilimali ya Joto Ardhi Nchini




## Kuratibu, Kusimamia na Kufuatilia Utekelezaji wa Programu na mikakati mbalimbali katika Sekta ya Umeme

| MIRADI | THAMANI YA MRADI | FEDHA ZILIZO-TENGWA 22/23 (Shilingi) |
|---|---|---|
| Mradi wa kuhamasisha matumizi endelevu ya nishati safi ya kupikia (Intergrated Approach to Sustainable Cooking Solutions) | Euro milioni 30 | Bilioni 1.00 |
| Mpango wa Kitaifa wa matumizi bora ya Nishati (The National Energy Efficiency Action Plan) | Euro milioni 9 | Bilioni 11.71 |

## Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia Udhibiti wa Shughuli za Mkondo wa juu

| MRADI | FEDHA ZILIZOTENGWA 22/23 (Shilingi) |
|---|---|
| Udhibiti wa Shughuli za Mkondo wa Juu wa Mafuta na Gesi Asilia. Serikali kupitia PURA itaanza maandalizi ya kunadi vitalu vilivyo wazi katika maeneo ya nchi kavu na baharini kwa kutumia mikataba maalum. Miongoni mwa maandalizi hayo ni pamoja na: kuchakata upya data za mitetemo zilizopo katika maeneo yaliyo wazi ya nchi kavu na kukusanya data za mitetemo za mfumo wa 3D kwa maeneo ya bahari kuu (Interactive Digital Petroleum Activities Map) | Bilioni 1.69 |

## Ramani ya Vitalu vya Mafuta na Gesi




## Miradi ya Utafutajwa Mafuta na Gesi Asilia Katika Vitalu vya Kimkakati

| MIRADI | FEDHA ZILIZOTENGWA 22/23 (Shilingi) |
|---|---|
| Kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini | Bilioni 83.67 |
| Kitalu cha Eyasi - Wembere | Bilioni 15.41 |
| Kitalu cha Songo Songo Magharibi (Drilling Management Consultant) | Bilioni 2.902 |
| Kitalu cha Ziwa Tanganyika (2D seismic plan and design) | Milioni 187 |
| Vitalu Namba 4/1B and 4/1C (kukusanya, kuchakata na kutafsiri taarifa za mitetemo katika vitalu tajwa na upatikanaji wa leseni na kumpata mbia ambaye atashirikiana na TPDC) | Million 5. Hiki ni kiasi cha kulipia cheti cha mazingira wakati mpango wa kumpata strategic partner ukiendelea. |
| Kitalu cha Ruvu (Kukamilisha ukusanyaji, uchakataji na kutafsiri data za mitetemo za mfumo wa 3D na kuanza kazi ya uchorongaji wa Kisima cha utafutaji katika maeneo ya Bagamoyo) | Serikali, TPDC na Dodsal wana mkataba wa Uzalishaji, ugawanaji mapato (PSA) ambapo ushiriki wa TPDC utakuwa kwa njia ya carried interest |
| Kitalu cha Ruvuma (Kukamilisha uchakataji wa data za mitetemo za mfumo wa 3D ili kuhakiki uwepo wa gesi asilia maeneo mengine na kuandaa taratibu za kuweza kuzalisha gesi iliyogundulika katika maeneo ya Ntorya) | Serikali, TPDC na ARA Petroleum wana mkataba wa Uzalishaji, ugawanaji mapato (PSA) ambapo ushiriki wa TPDC utakuwa kwa njia ya carried interest |
| Kitalu cha Kilosa - Kilombero (Kukamilisha kuchakata data za mitetemo na kuandaa maeneo ya uchorongaji wa visima vya utafuataji) | Serikali, TPDC na Swala Energy wana mkataba wa Uzalishaji, ugawanaji mapato (PSA) ambapo ushiriki wa TPDC utakuwa kwa njia ya carried interest. |
| Kitalu Namba 1& 4 na kitalu Namba 2 (kukamilisha majadiliano ya mkataba wa HGA, kufanya tafiti mbalimbali za kitaalamu zikiwemo usanifu wa awali wa kihandisi wa mradi (Pre-FEED)) | Serikali, TPDC, Shell kwa Kitalu Nambari 1 & 4 na Equinor kwa kitalu nambari 2 wana mikataba ya Uzalishaji, ugawanaji mapato (PSA) ambapo ushiriki wa TPDC utakuwa kwa njia ya carried interest |
| Kitalu cha Songo Songo (kuendelea na uzalishaji wa gesi asilia kwa ajili ya matumizi mbalimbali hapa nchini) | Serikali, TPDC na PAET wana mkataba wa Uzalishaji, ugawanaji mapato (PSA) ambapo ushiriki wa TPDC utakuwa kwa njia ya carried interest |
| Kitalu cha Mnazi Bay (TPDC wataendelea na kazi ya ukarabati wa visima na kufungua zones mpya) | Serikali, TPDC na Maurel & Prom wana mkataba wa Uzalishaji, ugawanaji mapato (PSA) ambapo wa ushiriki wa TPDC ni asilimia 20%. |

## Kuchakata Na Kusindika Gesi Asilia

| MIRADI | FEDHA ZILIZOTENGWA 22/23 (Shilingi) |
|---|---|
| Mradi wa Kuchakata na kusindika Gesi Asilia kuwa kimiminika (Liquefied Natural Gas - LNG) | Billioni 4.70 |
| Mpango wa Kufanya Eneo la Mradi wa LNG kuwa Ukanda Maalum wa Kiuchumi (Special Economic Zone) | TPDC itawasiliana na Halmashauri ya Mji wa Lindi namna ya uendelezaji wa Eneo la Mradi kuwa Ukanda Maalum wa Kiuchumi |

# TANGAZO

## Miradi ya Ujenzi wa Miundombinu ya Usafirishaji na Usambazaji wa Gesi Asilia

| MIRADI | FEDHA ZILIZOTENGWA 22/23 (Shilingi) |
|---|---|
| Usambazaji wa Gesi Asilia Katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani | Bilioni 3.89 |
| Kuunganisha Gesi Asilia Viwandani | Bilioni 5.15 |
| Usambazaji wa Gesi Asilia Katika Mikoa ya Lindi na Mtwara | Bilioni 5.49 |

## Mradi wa Vituo vya Nishati Mbadala

| MIRADI | FEDHA ZILIZOTENGWA 22/23 (Shilingi) |
|---|---|
| Ujenzi wa Vituo vya Gesi (CNG) katika Bohari za Mafuta za Serikali Dar es Salaam | Bilioni 1 |
| Ujenzi wa Kituo Mama na Vituo Dada vya Gesi (CNG) Katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani | Bilioni 23.2 |




Kituo cha Gesi - Dar es Salaam


## Miradi ya Kusafirisha Gesi Asilia kwa Nchi za Jirani

| MIRADI | FEDHA ZILIZOTENGWA 22/23 (Shilingi) |
|---|---|
| Mradi wa Bomba la Kusafirisha Gesi Kutoka Tanzania hadi Uganda (Upembuzi Yakinifu) | Milioni 635.02 |
| Mradi wa Kusafirisha Gesi Asilia Kutoka Dar es salaam (Tanzania) hadi Mombasa (Kenya) | Milioni 656.10 |

## Miradi ya Kusafirisha na Kuhifadhi Mafuta kwa nchi za Jirani

| MIRADI | FEDHA ZILIZOTENGWA 22/23 (Shilingi) |
|---|---|
| Mradi wa Bomba la Kusafirishia Mafuta Ghafi kutoka Hoima- Uganda hadi Tanga - Tanzania (East Africa Crude Oil Pipeline EACOP) - Kulipa fidia | Bilioni 5.50 |
| Mradi wa Bomba la Kusafirishia Mafuta Safi Kutoka Dar es salaam - Tanzania hadi Ndola- Zambia. | Milioni 500.00 |

## Ramani ya Njia ya Bomba la Mafuta la Mradi wa EACOP




## Mradi wa Kimkakati wa kuhifadhi Mafuta

(Strategic Petroleum Reserves- Spr)


Serikali ipo katika ukamilishaji wa kuwepo kwa hifadhi ya kikakati ya mafuta (Strategic Petroleum Reserves). Kusudi kubwa la kuwepo kwa SPR ni pamoja na kuendelea kuhakikisha usalama wa mafuta nchini (security of supply), lakini pia kuhimilisha bei za mafuta zinapobadilika hasa kwa kupanda juu. Serikali inaendelea kukamilisha urekebishwaji wa Kanuni (Regulations) zitakazoongoza utendaji wa huduma hii ya hifadhi ya mkakati ya mafuta. Huduma hii itasimamiwa na Shirika la Maendeleo ya Mafuta nchini (TPDC).

## Mfuko Wa Kuhimili Ukali Wa Bei Za Mafuta

(FUEL PRICE STABILIZATION FUND)

Serikali kupitia Wizara ya Nishati itaanzisha mfuko maalumu wa kuhimili ukali wa bei za mafuta (Fuel Price Stabilization Fund). Mfuko huu ambao utajengwa kwa utaratibu wa kujitegemea katika kupata fedha (self funding) kutokana na ubadilikaji wa bei za mafuta katika soko la dunia, utakuwa na lengo la kupunguza ukali wa bei za mafuta zinapopanda zaidi ya kiwango cha juu kitakachowekwa na kukubalika.

# TANGAZO




**Mwenendo wa bei za mafuta nchini kulinganisha na mafuta ghafi duniani.**

## Kuanzishwa kwa Maghala ya Kupokea Mafuta kwa mara moja
(SINGLE RECEIVING TERMINALS - SRT)

Serikali kupitia Wizara ya Nishati inakamilisha utaratibu wa upokeaji wa mafuta ya petroli kwa mara moja katika maghala ya TIPER. Hii itahusisha pia kuongeza maghala ya kupokea mafuta hapo TIPER na kuweka na kuimarisha miundombinu ya upokeaji mafuta ikiwemo kuweka boya la mafuta ya petroli (SBM) na mabomba ya upokeaji wa mafuta kutoka katika meli na pia mabomba ya utawanyaji wa mafuta katika maghala mengine. Mradi huu utahusisha pia ushiriki wa sekta binafsi kwa ushirikiano na Serikali.

Lengo la kuanzishwa kwa huduma hii ya SRT ni kuwezesha kupunguza muda wa meli unaotumika kwa sasa kwa kupakua mafuta ktk maghala mengi na hivyo kusababisha kuongezeka kwa gharama za meli kuwepo ktk sehemu ya kupakulia mafuta (demurrage). Gharama hizi huingizwa ktk bei za mafuta. Hivyo kupungua kwa gharama hizi kutasaidia kupungua kwa bei za mafuta kwa mtumiaji wa mwisho.

## Maghala ya Forodha kwa Ajili ya mafuta
(CUSTOMS BONDED WAREHOUSE)

Serikali kupitia wizara ya nishati inakamilisha taratibu za kuwezesha maghala ya mafuta ya TIPER na GBP (Tanga) kuwa maghala ya forodha ya mafuta (customs bonded warehouses). Hii itasaidia nchi yetu kuwa kitovu (hub) cha mafuta katika ukanda huu wa Afrika ikiunganishwa na ujenzi wa maghala mengine hapo TIPER. Aidha, hatua hii itawezesha pia kufanyika kwa biashara ya uuzaji wa mafuta katika meli zinazokuja katika mwambao huu (bunkering business). Biashara ambayo kwa sasa inafanyika kupitia bandari ya Mombasa au Afrika Kusini katika ukanda huu.

Pamoja na huduma hii kuwezesha kuwa kitovu cha mafuta (hub) kwa ukanda huu, lakini pia huduma hii itakuwa ni njia nyingine ya kuwepo kwa usalama wa upatikanaji wa mafuta nchini (security of supply of petroleum products).

## Ushiriki wa TPDC Katika Biashara ya Mafuta Kupitia TANOIL

| MIRADI | FEDHA ZILIZOTENGWA 22/23 |
|---|---|
| Kuimarisha Mtandao wa Usambazaji TPDC kupitia TANOIL itajenga na kukarabati vituo vyake vinne vya mafuta vya Segera (Tanga), Makuyuni (Arusha), Tarime na Musoma (Mara) | Bilioni 2.04 |
| Kukarabati Tenki Namba 8 penye uwezo wa tani 45,000 linalomilikiwa na TPDC lililopo ndani ya hifadhi ya TIPER pamoja na matenki mengine yaliyopo katika eneo la TPDC Kigamboni | Bilioni 12.11 |
| Katika kutatua wigo wa biashara, TANOIL imepanga kununua maeneo kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya mafuta kwa kushirikiana na Halmashauri za Manispaa na Wilaya, pia kuingia ubia na wawekezaji ambao watawekeza katika ujenzi huo. | Bilioni 2.5 |




Kituo cha Mafuta cha TANOIL - Mkoani Iringa.

## Mipango na mikakati ya Wizara na Taasisi zake

1. Mkakati wa Nishati Jadidifu (Renewable Energy Strategy and Roadmap),
2. Mkakati wa Matumizi Bora ya Nishati na Mpango wa Utekelezaji (Energy Efficiency Strategy and Its Implementation Action Plan)
3. Mkakati wa Tungamotaka (Biomass Energy Strategy).
4. Wizara pia itafanya mapitio ya Sekta ya Umeme (Power System Master Plan)
5. Kutekeleza Mpango Kabambe wa Nishati Vijijini (Rural Energy Master Plan)
6. Mpango wa Nishati Safi ya Kupikia Vijijini.
7. EWURA na PURA imeanzisha Kanzi Data ya Wataalam wa ndani (Tanzania Professionals Database - TPD)

8. Kuanzisha Mfuko wa Kudhibiti Mabadiliko ya Bei za Mafuta (Fuel Price Stabilization Fund – FPSF)
9. Kuanzisha Hifadhi ya Mafuta ya Kimkakati (National Strategic Petroleum Reserve)

## Jumla Ya Bajeti Ya Wizara Ya Nishati Na Taasisi Zake Kwa Mwaka 2022/23.

Katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo na Shughuli za Wizara za kawaida katika Mwaka wa Fedha 2022/23 , Serikali imetenga Bajeti ya jumla ya Shilingi 2,705,981,533,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:

- Shilingi 2,676,229,576,000 sawa na asilimia 99 ya Bajeti yote ya Wizara ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi 2,508,756,128,000 ni fedha za ndani na Shilingi 167,473,448,000 ni fedha za nje; na

- Shilingi 29,751,957,000 sawa na asilimia 1 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo Shilingi 15,025,821,000 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na Shilingi 14,726,136,000 kwa ajili ya Mishahara (PE) ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini zake

**Wizara ya Nishati**
Mtaa wa Nishati, Mji wa Serikali Mtumba
S.L.P 40474, Dodoma

+255 26 2322018

**ps@nishati.go.tz**



# Bilioni 4/- zatengwa utambuzi wa ardhi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imesema inakusudia kutekeleza mradi mkubwa wa utambuzi wa ardhi ambao umetengewa Sh. bilioni nne na utawawezesha wananchi kupata hatimiliki na kuondokana na migogoro ya ardhi.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, alisema hayo jana wakati akitoa ufafanuzi kuhusu mikakati inayochukuliwa na wizara katika kulipatia ufumbuzi tatizo la ardhi na migogoro yake.

Alisema kutofanyika kwa utambuzi wa ardhi ni moja ya sababu kubwa zinazoibua migogoro ya ardhi pamoja na wananchi kuvamia eka tatu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za kudumu.

Ili kuondokana na migogoro na mivutano hiyo, alisema utambuzi wa ardhi ambao utawapatia wananchi hatimiliki ndilo ufumbuzi pekee wa kuondosha malalamiko hayo.

"Mheshimiwa Spika napenda niwajulishe wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba serikali imetenga Sh. bilioni 4 kwa ajili ya kutekeleza utambuzi wa ardhi ikiwamo kuwapimia ardhi pamoja na utoaji wa hatimiliki. Hatua hii inakwenda moja kwa moja kujibu migogoro na mivutano katika umiliki wa ardhi," alisema.

Alikiri kuongezeka kwa migogoro hiyo zaidi katika maeneo ya ukanda wa pembezoni mwa bahari kutokana na ardhi kuongezeka thamani siku hadi siku kutokana na kasi ya uwekezaji katika sekta ya utalii.

Pia Dk. Salum alisema utambuzi wa ardhi pia utasaidia kuwawezesha wananchi kupata umiliki wa ekari tatu ambazo zilitolewa na rais wa kwanza wa Zanzibar, Sheikh Abeid Amani Karume.

Alisisitiza kuwa msimamo wa serikali ni kwamba ekari tatu haziuzwi isipokuwa zitabakia kwa matumizi ya shughuli za kilimo kwa wananchi.

**Alisema kutofanyika kwa utambuzi wa ardhi ni moja ya sababu kubwa zinazoibua migogoro ya ardhi pamoja na wananchi kuvamia eka tatu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za kudumu**

# Kampuni yaomba kulipa kodi gari la kifahari kwa awamu

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Turky Mifuko Zanzibar imeomba kulipa kodi kwa awamu baada ya maombi ya msamaha wa kodi ya Sh. milioni 308.5 kukataliwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Zanzibar, Juma Bakari Hassan, alisema kampuni inayomilikiwa na mfanyabiashara Toufky Salum Turky, imewasilisha maombi ipewe nafasi ya kulipa kwa awamu tatu kiwango hicho cha kodi.

"Baada ya kumpa siku saba awe amelipa, ameleta barua ya maombi akitaka alipe kidogo kidogo kwa awamu tatu kwa madai ya kwamba hali ya kifedha si nzuri na tunatarajia kumjibu maombi yake," alisema.

Naibu Kamishna huyo alisema gari hilo la kifahari aina ya Benzi, liliingizwa Zanzibar Januari, mwaka huu, na kutolewa bandarini na kampuni ya uwakala wa forodha ya Zara Freight Forwarders yenye makao makuu Malindi, Zanzibar kupitia Bandari ya Malindi.

"Gari aina ya Benz lilitolewa kwa maombi ya msamaha wa kodi baada ya kampuni ya Turkey Mifuko Zanzibar kuwasilisha maombi yake kwa Waziri wa Fedha. Mara ya kwanza yalikataliwa na mara pili yamekataliwa licha ya Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) kuwatetea kuwa wanahaki ya kupewa msamaha," alisema Hassan. Alisema kwa msingi huo, kampuni hiyo inatakiwa kulipa kiwango chote cha kodi kilichotakiwa licha ya gari hilo kutolewa bandarini kwa dhamana ya bondi ya bima na kama itashindwa kutekeleza kuna hatua za kisheria zitachukuliwa kutokana na dhamana waliyoitumia.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), Ahmed Makarani, alisema tayari wamefungua jalada la uchunguzi kwa tuhuma za kukwepa kodi na uchunguzi unaendelea.

"Tunaendelea na uchunguzi kuhusu gari aina ya Benz ambalo liliingizwa bila kulipiwa kodi. Uchunguzi ukikamilika jalada litapelekwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kabla ya hatua zingine za kisheria," alisema Makarani.



Mkulima mwani, Fatma Machano, akipiga makasia wakati akitoka kwenye shamba lake la mwani katika kijiji cha Tumbe, Pemba jana, ambapo sasa wanalima katika kina kirefu cha maji kutokana na mabadiliko ya tabianchi yaliyoathiri zao hilo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mabadiliko tabianchi yaathiri mwani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KUTOKANA na mabadiliko ya tabianchi, uzalishaji wa mwani katika kina kifupi cha maji ya bahari umeathirika, hivyo wakulima wa kilimo hicho Kisiwani Pemba wamelazimika kuhamia katika kina kirefu.

Hayo yalielezwa hivi karibuni na Ofisa Kilimo cha Mwani kutoka Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi, Asha Khamis, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika ziara maalum kwa wakulima wa mwani wa kijiji cha Tumbe, Pemba.

Ziara hiyo iliandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) kwa ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Marekani (USAID) kupitia mradi wa Tuhifadhi Maliasili.

Alisema kilimo hicho kinakabiliwa na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi yaliyochangia kiwango kidogo cha uzalishaji kwa sababu ya kupanda joto la bahari, hivyo mwani kuharibika.

Mabadiliko ya tabianchi, alisema yamesababisha mwani kutoota katika kina kifupi cha maji na sasa wakulima wamehamia katika kina kirefu cha maji, ambako ni shida kufika.

Pia ofisa huyo alisema serikali inachukua hatua kuboresha kilimo cha mwani ambapo miongoni mwa juhudi hizo ni kuwapatia wakulima boti 500 kupitia fedha za ahueni za Covid-19 ambazo zitawezesha wakulima kulima mwani katika kina kirefu.

Naye mkulima wa mwani wa kijiji cha Tumbe, Fatma Machano Ali, alisema ili kufika katika kina kirefu cha maji, mkulima anatakiwa kuwa na boti, ujuzi wa kuogelea, jaketi la uokozi na vifaa vya kujilinda dhidi ya viumbe hatari baharini.

Alisema ili mkulima kuwa na usafiri wa uhakika wa kufikia shamba la mwani, anahitaji kuwa na wastani wa Sh. milioni 6.5 kununua boti na vifaa vyake.

"Kwa sababu hatuna boti za kutufikisha kina kirefu cha maji, tunalazimika kuomba msaada wa usafiri kutoka kwa wavuvi," alisema.

Pia alisema wanahitaji elimu ya ujuzi wa kuogelea ili kunusuru maisha yao wakati wa dharura.

Alisema wakati akilima katika kina kifupi cha maji uzalishaji ulikuwa mdogo ambapo kwa bamvua (msimu) alikuwa akivuna robo tani lakini kwa sasa ana uwezo wa kuvuna hadi tani moja.

Tani moja ya mwani ni sawa na kilo 1,000 ambapo kilo moja ya mwani mkavu kwa sasa inauzwa Tsh. 600 katika masoko ya ndani.

Fatma, alisema ana uwezo wa kupata zaidi ya Sh. 600,000 kwa miezi mitatu sawa na mshahara wa kima cha chini kwa mtumishi wa umma kwa miezi miwili.

Mkurugenzi Mtendaji wa JET, John Chikomo, alisema chama hicho kinaendelea kuwejengea uwezo waandishi wa habari ili kuwa na ujuzi wa kuandika habari za mazingira zenye tija kwa Watanzania wakiwamo wakulima wa mwani.

"JET inaendelea kutafuta fursa mbalimbali kuhakikisha mazingira yanalindwa na kuhifadhiwa yakiwamo mazingira ya bahari ambayo ni rasilimali tegemezi kwa wananchi wakiwamo wakulima wa mwani," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**SADA I. KAGALWE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye Index namba **S.3714/0018** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MATWIGA SEKONDARI mwaka 2016. Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **DAR/CHU/RB/210309/2022.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**CLET AZIZ BABU,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu kidato cha nne index No **S.0486/0046** Mwaka 2014 Shule ya Sekondari **UOMBONI,** kilichotolewa na Baraza la mitihani la Taifa. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa polisi: **MWA/NYA/RB/208483/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SYLEVESTER CHACHA RIOBA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya LANDROVER yenye usajili namba **T649 AJS,** yenye CHASSIS NAMBA: **SALLDHMC7A383094** na ENGINE NAMBA :**12142994C.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA :
**DAR/URA/RB/216735/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**BEATRICE JOHN KAPITINGANA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya TVS yenye namba za usajili **MC690CPA.** Chassis No. **MD625AF78L1A00438,** Engine No. **AFZAL1200400.** **Y**eyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**DOD/DOD/RB/214493/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**WENDE LAISON MLELWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA HARRIER** yenye namba za usajili **T 470 DFU,** Lenye chassis namba **MCU 1500096341** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi. TAARIFA
**POLISI:IRI/IRI/RB/37328/2022**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA -MWANZA**

**SHAURI NA.305 LA 2021**

**SHEKHA SALIM....................................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**ZIADA SADICK.....................................WAJIBU MAOMBI**

**WITO WA KUITWA BARAZANI**

**KWA ZIADA SADICK**

Unafahamishwa kwamba mleta maombi hapo juu amefungua Shauri/Ombi dhidi yako katika Baraza la Ardhi na Nyumba Mkoa wa Mwanza,ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 23/05)2022 katika Chumba Cha BARAZA Na.1,Barabara ya Makongoro Jengo liko Mkabala na Mahakama ya Mwanzo Nyamagana Mjini,TANZANIA.

Kwa hivyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza siku hiyo wewe mwenyewe,wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria kujibu ombi hili.
KAA- Ukijua kwamba kushindwa kufika,Baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila wewe kuwepo.

Imetolewa nami kwa Amri na Chapa ya Baraza leo tarehe 11/05/2022.

MAYEYE S.M
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
MWANZA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ............TANGA**

**Kituo cha..... MJINI TANGA.... Mkoa... TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi Na:......112/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**

**MAREHEMU: HABIBU ABDALLAH HABIBU**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA**

**MSIMAMIZI YALIYOLETWA**

**NA: IBRAHIMU HABIBU ABDALLAH**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslai yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 21/6/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

Imetolewa leo **31/05/2022**

HAKIMU

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
TANGA MJINI

Uza, Chenye Thamani Kubwa
Kwa Kutangaza Nasi
Kwa Bei Poa
Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Uingereza kuanza kuwahamishia Rwanda wahamiaji wiki ijayo

**LONDON, Uingereza**

NDEGE ya kwanza kuelekea nchini Rwanda ikiwa na wahamiaji walioingia Uingereza kwa njia ya baharini, inatarajiwa kuondoka Juni 14, mwaka huu.

Ofisi ya Mambo ya Ndani ya Uingereza, ilisema maofisa wameanza kutoa maelekezo rasmi kwa watu wa kwanza kupelekwa katika nchi hiyo ya Afrika.

Inatarajiwa kuibuka kwa changamoto za kisheria dhidi ya hatua hiyo.

Mpango huo wenye utata umekosolewa na wanasiasa, mashirika ya misaada na Askofu Mkuu wa Canterbury ambaye aliuita kinyume cha asili ya Mungu.

Chini ya mpango huo, baadhi ya waomba hifadhi ambao wamewasili Uingereza watapelekwa Rwanda ambako maombi yao yatashughulikiwa.

Wakati maombi yao yanachambuliwa watapewa malazi na usaidizi, ikiwa watafaulu wataweza kusalia Rwanda na kupata elimu na usaidizi hadi miaka mitano.

Katibu wa Mambo ya Ndani Priti Patel, alisema ushirikiano na Rwanda ni sehemu muhimu ya mkakati wetu wa kurekebisha mfumo uliovunjwa wa hifadhi.

**BBC**

**Wakati maombi yao yanachambuliwa watapewa malazi na usaidizi, ikiwa watafaulu wataweza kusalia Rwanda na kupata elimu na usaidizi hadi miaka mitano.**

# Russia yadhibiti 70% Severodonetsk, yaionya Marekani itajiongezea hatari

**KYIV, Ukraine**

UKRAINE imethibitisha kuwa vikosi vya Russia vinadhibiti takribani asilimia 70 ya mji wa Severodonetsk, wakati Marekani na Ujerumani zikitangaza kupeleka nchini humo mifumo ya kisasa ya kurushia makombora ya kujilinda.

Akizungumza siku ya Jumatano, Gavana wa jimbo la Luhansk, Serhiy Gaidai alisema mapigano yanapamba moto, lakini Russia inajaribu kudhibiti eneo la mashariki la Luhansk.

Kauli hiyo aliitoa kupitia mtandao wa mawasiliano wa Telegram, na kusema kwamba baadhi ya wanajeshi wa Ukraine wamerudi nyuma, baada ya mashambulizi kuongezeka katika mji wa kimkakati wa Severodonetsk.

Alisema mapigano katika mji huo yaliongezeka mara dufu siku mbili za Mei 30 na 31.

Severodonetsk ni mji mkuu wa jimbo la Luhansk ndiyo eneo la mwisho katika jimbo hilo ambao unadhibitiwa na vikosi vya jeshi la Ukraine.

**UJERUMANI KUPELEKA MIFUMO YA KUZUIA MASHAMBULIZI**

Kansela wa Ujerumani, Olaf Scholz amesema nchi yake itapeleka Ukraine mifumo ya kisasa ya roketi za kuzuia mashambulizi ya anga, aina ya IRIS-T.

Akilihutubia bunge la Ujerumani, Bundestag Jumatano, Scholz alisema nchi yake iliahidi kuipatia Ukraine mfumo wa rada wenye uwezo wa kufuatilia na kugundua ndege za adui, roketi pamoja na makombora.

"Pia tutapeleka silaha zaidi katika wiki zijazo. Kwa mfano, serikali ya Ujerumani imeamua kwamba tutapeleka mfumo wa IRIS-T, mfumo wa kisasa zaidi wa kujilinda na mashambulizi ya anga. Itaisaidia Ukraine kujilinda na mashambulizi ya anga ya Russia," alifafanua Scholz

Kansela huyo aliutangaza mpango huo, muda mfupi baada ya Rais wa Marekani, Joe Biden naye kusema ataipatia Ukraine mifumo ya kisasa ya makombora, wakati vikosi vya Russia vinajaribu kuuteka mji muhimu wa mashariki ya Ukraine.

Mifumo hiyo ni sehemu ya msaada wa euro milioni 653 wa silaha unaotarajiwa kutangazwa ,

Msaada huo wa usalama unajumuisha helikopta, mifumo ya silaha za kuzuia mashambulizi ya vifaru, magari ya kijeshi, mfumo wa rada na magari ya kivita.

**RUSSIA YAIONYA MAREKANI INAZIDISHA HATARI KUJIINGIZA VITANI**

Russia imejibu kuwa mpango wa Marekani kupeleka silaha mpya Ukraine pamoja na mifumo ya kuzuia mashambulizi, unaongeza hatari ya nchi hiyo kujiingiza moja kwa moja kwenye mzozo na Russia.

Naye kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis amewasihi viongozi kuondoa vizuizi vya mauzo ya ngano kutoka Ukraine, akisema kwamba nafaka hiyo haiwezi kutumika kama silaha ya kivita.

Akizungumza mbele ya maelfu ya waumini katika uwanja wa Kanisa la Mtakatifu Peter, Vatican, Papa Francis alisema vizuizi hivyo vinapaswa kuondolewa kwa sababu mamilioni ya watu hasa katika nchi masikini zaidi duniani wanategemea ngano kutoka nchi hiyo.

Wakati huo huo, Shirika la Umoja wa Mataifa la kuwahudumia watoto, UNICEF limesema zaidi ya watoto milioni tano wa Ukraine wanategemea msaada wa chakula.

Ndani ya Ukraine kwenyewe, watoto milioni tatu wanahitaji msaada na wengine milioni 2.2 waliokimbia vita wanahitaji pia msaada.

Kwa mujibu wa UNICEF, watoto wapatao 262 wameuawa tangu vita vilipoanza na mamia ya shule zimeharibiwa. ***DW***



Waasi wa kundi la M23 wakiondoka eneo la Mashariki ya DRC hivi karibuni. **PICHA: AP**

# Rwanda yatishia kuingia vitani ikichokozwa

**KIGALI, Rwanda**

HALI inazidi kuwa mbaya na hofu ya kuibuka vita baada ya Rwanda kusema iko tayari kulipiza kisasi iwapo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo itashambulia tena.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Rwanda, Dkt Vincent Biruta amekilaumu kikosi cha Umoja wa Mataifa (MONUSCO) kufumbia macho uchokozi huo, huku ikishirikiana na waasi wa FDLR wanaohusishwa na mauaji ya kimbari wanaotaka kuipindua serikali ya Rwanda.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini Kigali, Waziri huyo alisema Jeshi la Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo lilirusha mabomu ndani ya Rwanda Mei 19 na 23 , lakini nchi hiyo haijaomba msamaha.

Biruta alisema kuwa DRC inataka kuwavuta kwenye vita yao kwa kuwarushia mabomu pale wapotaka.

Aliongeza kwamba waliwauliza kulikoni lakini hawajakiri kosa na wala hawajawaambia hatua walizochukua kusitisha uchokozi huo.

Alilisitiza kwamba Rwanda inataka amani, hawataki vita na hawafahamu kwanini DRC inataka mapigano.

Uhusiano kati ya nchi hizo mbili uliingia doa baada ya kuibuka mapigano mapya kati ya Jeshi la DRC na waasi wa M23 ambao Rwanda inadaiwa kuwafadhili.

Rwanda nayo inaituhumu DRC kwa kulifadhili kundi la FDLR lenye lengo la kuipindua serikali ya Rwanda. Rwanda ilisema endapo itaendeleza uchokozi huo na jirani yake akikataa kuwaachia wanajeshi wawili wa Rwanda inaowashikilia itajibu mapigo.

Biruta aliendelea kusema serikali yake ina jukumu la kuwalinda wananchi wao na mipaka yao na kuongeza kuwa nchi ikivamiwa itajitetea.

Waziri huyo aliongeza kwamba wana haki kama ilivyo kwa nchi zingine zote na endapo usalama wao utaendelea kuhujumiwa watajilinda.

Aidha, alilaumu jeshi la DRC na lile la Umoja wa Mataifa (MONUSCO) kushirikiana na waasi wa FDLR katika vita dhidi ya M23, wakati makundi yote wana jukumu la kuyasambaratisha.

***DW***

## HABARI MICHEZO



Baadhi ya wananchi wakiwa katika foleni ya kuelekea kupiga picha ya kumbukumbu na Kombe la Dunia katika siku ya pili ya ziara ya kombe hilo nchini kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

# COCA-COLA YAKUSANYA MAELFU KOMBE LA DUNIA KWA MKAPA

**Na Mwandishi Wetu**

MAELFU ya Watanzania, jana wamejitokeza kwa wingi kushuhudia na kupiga picha na Kombe Halisi la Dunia la FIFA lililoletwa nchini chini ya Kampuni ya Coca-Cola Tanzania, hafla iliyofanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ikipambwa na burudani kutoka kwa wasanii mbalimbali, na uoneshwaji wa Filamu ya Royal Tour.

Kombe la Dunia lilitua nchini juzi alfajiri, ambapo lilipokelewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, Ikulu jijini Dar es Salaam, kabla ya jana kupelekwa Uwanja wa Mkapa kuruhusu Watanzania kupiga nalo picha, dhifa hiyo ikipambwa na wasanii mbalimbali wa kizazi kipya, wakiwamo Chegge Chigunda na Mr. Bluu.

Wakali wengine waliopamba masaa sita ya hafla hiyo ni Mzee wa Bwax, Sholo Mwamba, Juma Nature na Kala Pina, ambao walikuwa ni miongoni mwa wasanii waliotumbuiza, kuhitimisha siku mbili za ziara ya Kombe la Dunia nchini, iliyofanyika kwa udhamini wa Kampuni ya Coca-Cola Tanzania.

Aidha, serikali imeipongeza Coca-Cola Tanzania kwa kufanikisha ujio wa ziara ya Kombe halisi la Dunia la FIFA, huku ikiahidiwa kuitumia ziara hiyo kama chachu ya uboreshaji miundombinu ya soka, ili sio tu kuiwezesha Tanzania kuomba uwenyeji wa AFCON 2027, bali pia kuharakisha ukuzaji vipaji vya mchezo huo.

Hayo yamesemwa na Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Pauline Gekul, wakati wa hafla ya Chakula cha Usiku cha waalikwa Maalum wa ziara ya Kombe la Dunia (FIFA Trophy Tour Night Gala), iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi usiku, ikihudhuriwa na zaidi ya watu 300 walioalikwa na Coca-Cola Tanzania.

Naibu Waziri Gekul alibainisha kuwa, Kampuni ya Coca-Cola na Shirikisho la Soka Duniani (FIFA), limewashika mkono Watanzania, ambao wanapaswa kusapoti jitihada za serikali yao katika kufanikisha kasi ya ukuaji na uendelezaji wa vipaji nchini, sambamba na ujenzi wa miundombinu inayokidhi viwango vya kimataifa.

"Rais Samia Suluhu Hassan ametamka mchana wakati ziara hii ilipofanyika Ikulu, waziri naye akakazia, nami niseme hapa hadharani kwamba, thamani hii tuliyopewa na Coca Cola Tanzania na FIFA, ya kuwa moja kati ya mataifa manne yasiyofuzu fainali za Qatar kutembelewa na kombe hili, tunapaswa kuienzi kwa vitendo.

"Watanzania wawe na imani na serikali, wizara na mipango chanya ya Rais Samia katika sekta ya michezo. Tuko kazini kuhakikisha mipango hii endelevu ya kustawisha soka letu, inatekelezeka na kuzaa matunda. Tuwahakikishie kuwa yaliyotamkwa yako kwenye utekelezaji na hivyo Watanzania wajue tuna kazi ya kufanya.

"Kama serikali tunatumia chachu hii iliyoletwa na Coca-Cola, kuhakikisha tunapita mkoa kwa mkoa, wilaya kwa wilaya, kata ama kijiji kwa kijiji, mtaa kwa mtaa kustawisha soka, ili miaka michache ijayo tusiwe miongoni mwa nchi zinazoletewa kombe hili zikiwa hazijafuzu fainali, bali lije tukiwa na tiketi yetu mikononi," alisisitiza Gekul.

Naye Mkurugenzi Mwandamizi wa Masoko wa Coca-Cola Afrika, Nelly Wainaina, alisema wao kama Coca-Cola Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, wanajisikia furaha nchi zao mbili za Kenya na Tanzania kuwa mwenyeji wa ziara hiyo, ambayo Watanzania wanapaswa kuitumia kuamsha ari, kiu na hamasa ya maendeleo ya soka.

Aliushukuru msafara wa FIFA uliooongozwa na Juliano Belleti kwa kutua nchini salama na taji hilo, huku akizishukuru kampuni washirika wa Coca-Cola zikiwamo Nyanza Bottlers, Bonite Bottlers na kampuni zingine zinazoidhamini FIFA kwa kuwa sehemu muhimu ya ziara na kuhudhuria hafla hiyo usiku wa juzi.

Awali, mchana wakati wa hafla ya utambulisho wa ziara na taji la Dunia la FIFA kwa wanahabari, Meneja Mkuu wa Biashara wa Coca-Cola Tanzania, Hellen Masumba, alisema wanayo furaha kubwa kuwa sehemu ya kuwaletea Watanzania msisimko na shamrashamra za Kombe la Dunia.

"Kwa miaka mingi Coca-Cola wamekuwa washirika wa FIFA katika kuwapatia msisimko halisi kupitia ziara ya Kombe la Dunia la FIFA. Kuwasili kwa kombe bila shaka ni fursa ya aina yake kwa Watanzania kujumuika na dunia nzima kupitia ulimwengu wa mpira wa miguu ambapo wataweza kuliona kwa ukaribu zaidi.

"Ushirikiano wetu na FIFA katika kulileta kombe hili maarufu, ni ishara kwamba tunatambua na kuthamini kile wanachokiamini na kukipenda kwa dhati wateja na watumiaji wa bidhaa zetu hususan mchezo wa mpira wa miguu," alisisitiza Hellen kwa kuwakaribisha Watanzania jana katika Uwanja wa Taifa wa Benjamin Mkapa.

## Mwaikenda aongezwa Stars ikiifuata Niger leo

**Na Adam Fungamwango**

BEKI wa Azam FC, Lusajo Mwaikenda ameongezwa kwenye kikosi cha timu ya Taifa, Taifa Stars ambacho kinatarajiwa kuondoka leo kwenda nchini Benin kucheza mechi ya kwanza ya Kundi F dhidi ya Niger, kusaka tiketi ya kucheza fainali ya Mataifa ya Afrika (AFCON) 2023 zinazotarajiwa kuchezwa nchini Ivory Coast.

Meneja wa timu hiyo, Nadir Haroub 'Cannavaro', amesema mchezaji huyo ameongezwa na tayari yupo na wenzake kwa ajili ya safari kwenda kukipiga na timu hiyo katika mchezo utakaochezwa nchini Benin Jumamosi wiki hii.

Stars itakipiga dhidi ya Niger kwenye Uwanja wa L'Amitie jijini Cotonou, Benin, kwani timu hiyo haichezi nchini kwake kutokana na viwanja vya huko kutokidhi vigezo vya Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

"Mazoezi yanaendelea vizuri, vijana wametimia wote na kesho (leo), wanakwenda Benin kwa ajili ya kucheza mechi ya kutafuta nafasi ya kucheza fainali za Mataifa ya Afrika. Tumejipanda vizuri na safari hii tunataka pointi kwa kila tunayekutana naye. Mwaikenda amejiunga na wenzake na vijana wote wapo kambini," alisema nahodha huyo wa zamani wa Taifa Stars.

Mwaikenda, mwenye uwezo wa kucheza namba zote za ulinzi, pembeni na kati, ameongezwa kutokana na kuwapo kwa wachezaji majeruhi kama Shomari Kapombe wa Simba.

Stars ipo kwenye Kundi F, pamoja na timu za Niger, Argeria, na Uganda. Fainali za AFCON zinatarajiwa kuchezwa nchini Ivory Coast Juni 23 hadi Julai 23, mwakani.

## Ligi Kuu Z'bar kuendelea leo

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LIGI Kuu Zanzibar mzunguko wa 29, inatarajia kuendelea wiki hii katika Uwanja wa Gombani Kisiwani Pemba na Amaan, Unguja ambapo baada ya mechi hizo, itabaki raundi moja kabla ya ligi hiyo kufikia ukingoni msimu huu.

Ligi hiyo inaendelea wakati huu ambao tayari KMKM imeshatawazwa kuwa bingwa wa msimu huu wa 2021/22 huo ukiwa ni msimu wa pili mfululizo.

Katika mzunguko huu timu ya Mlandege FC itashuka dimbani kumalizana na Maafande wa JKU wakati Maafande wa Zimamoto wataoneshana ubabe na wenzao wa Polisi katika dimba la Amaan leo.

Kesho Maafande wa Uhamiaji watawakaribisha KVZ katika Uwanja wa Amaan majira ya saa 12 jioni wakati keshokutwa Wekundu wa Mjimkongwe timu ya Malindi wakikipiga na Wanajeshi wa Kipanga katika Uwanja wa Mau A kabla ya Juni 6, Taifa Jang'ombe kuhitimisha mzunguko huu wa 29 dhidi ya Black Sailor.

## ZISIKUPITE

### MOUNT ATAKIWA UNITED

KLABU ya Manchester United inafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Chelsea na England, Mason Mount, 23, ambaye bado hajasaini mkataba mpya pale Stamford Bridge. ***(Sun)***

### TERRIER KUMRITHI MANE

LIVERPOOL inamfuatilia mshambuliaji wa Rennes, Mfaransa Martin Terrier, 25, kama mbadala wa Sadio Mane, 30, iwapo mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal ataondoka Anfield. ***(Mirror)***

### XAVI AMTAKA NEVES

KOCHA wa Barcelona, Xavi amefanya mazungumzo na kiungo wa kati wa Wolves na Ureno, Ruben Neves, 25, kuangalia uwezekano wa kumsajili. ***(Sport)***

### LAPORTE AWINDWA JUVE

JUVENTUS wanaendelea kumtaka beki wa Manchester City, Aymeric Laporte, 28. ***(Corriere dello Sport via Manchester Evening News)***

### ZINCHENKO NA EBERTON

MLINZI wa kushoto wa Manchester City wa Ukraine, Oleksandr Zinchenko, 25, anazivutiwa klabu za Everton na Newcastle. ***(Sun)***

### AGUERD ATAKIWA LONDON

KLABU ya West Ham inakaribia kukamilisha mpango wa kumsajili beki wa Rennes, Nayef Aguerd, 26. 'Wagonga Nyundo' hao wa London pia walijaribu kumsajili mchezaji huyo wa Morocco msimu uliopita wa majira ya joto. ***(Evening Standard)***

### TIELEMANS ATAKIWA ARSENAL

KLABU ya Arsenal bado inamtaka kiungo wa Leicester City, Youri Tielemans, 25, huku Mbelgiji huyo akitarajiwa kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto, lakini klabu nyingine mbili pia ziko kwenye kinyang'anyiro cha kumwania. ***(Fabrizio Romano)***

### DEST AWINDWA CHELSEA

CHELSEA wamefufua nia yao ya kumsajili beki wa pembeni wa Barcelona na Marekani, Sergino Dest, 21. ***(Mail)***

### ALMIRON HAONDOKI

WAKALA wa Miguel Almiron, 28, amesisitiza kuwa mshambuliaji huyo wa Paraguay hataondoka Newcastle United msimu huu, huku kipengele chake cha kuachiliwa kikiripotiwa kuwa na thamani ya pauni milioni 60. ***(Chronicle Live)***

### LUKAKU KURUDI INTER

KLABU ya Inter Milan inatarajiwa kufanya mazungumzo na mwanasheria wa mshambuliaji wa Chelsea, Romelu Lukaku, 29, kuangalia namna mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji anavyoweza kurejea Serie A. ***(Guardian)***

### MAMADASHVILI ANUKIA SPURS

GOLIKIPA raia wa Georgia, Giorgi Mamadashvili mwenye umri wa miaka 21, ambaye kwa sasa anachezea kule Valencia, anasakwa na Tottenham Hotspur. ***(Marca)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# HAZARD HAJUI HATIMA YAKE UBELGIJI KOMBE LA DUNIA

**Sijajua bado kama nitaenda Qatar, sasa tuna wachezaji wakubwa na vijana ambao watajionyesha...**

**BRUSSELS,** Ubelgiji

EDEN Hazard amesema "natumaini bado sijamaliza" muda wa kucheza, lakini hajui mustakabali wake baada ya Kombe la Dunia akiwa na Timu ya Taifa ya Ubelgiji.

**Winga huyo wa Real Madrid amevumilia msimu mwingine wa kutatanisha, licha ya 'Los Blancos' kumaliza na taji la 35 la LaLiga na Kombe la 14 la Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kuwafunga Liverpool, Jumamosi iliyopita.**

Hazard alianza mechi saba pekee za LaLiga msimu huu kati ya 18, na alitoa pasi moja tu ya bao bila ya kufunga.

Huo umekuwa mtindo wa kukatisha tamaa kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, ambaye amefanikiwa kucheza mechi 48 pekee kwenye ligi akiwa na Madrid tangu aondoke Chelsea mwaka 2019.

Hazard anabaki kuwa nyota anayependwa sana katika chumba cha kubadilishia nguo cha Madrid, akionekana mara kwa mara akiwa amezungukwa na wachezaji wenzake kwenye sherehe mbalimbali za msimu huu, lakini anajitahidi kuimarika msimu ujao.

Kazi yake inayofuata ni kuiongoza Ubelgiji katika michuano ya Ligi ya Mataifa ya Uefa, kuanzia dhidi ya Uholanzi Ijumaa, na Hazard anatumaini kuisaidia nchi yake, ambayo itawania ubingwa wa Kombe la Dunia nchini Qatar.

"Nilisikitishwa na michuano ya Ulaya. Nilikuwa nimefanya kila niwezalo kujiweka sawa, lakini nikakosa nafasi dhidi ya Ureno," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Sasa tuna wachezaji wakubwa na vijana ambao watajionyesha, tunatakiwa kwenda Qatar tukiwa na matumaini ya kushinda, nataka niweze kucheza bila matatizo na kurejea katika kiwango changu cha zamani.

"Lakini sijajua bado nitaendelea baada ya Qatar, inategemeana na mambo mengi sana, familia yangu, lakini mwili wangu.

"Sijui kama nitacheza michezo yote. Usisahau kwamba nimecheza soka kidogo sana katika miezi ya hivi karibuni.

"Lakini nataka kutumia mechi hizi kurudi kwenye kiwango changu. Kimsingi, nitafanya maandalizi mazuri ili kucheza na kuwa imara kwa Kombe la Dunia."

Ingawa bado hana uhakika juu ya mustakabali wake wa Kombe la Dunia akiwa na Ubelgiji, Hazard amesisitiza kuwa atajitolea kwa kila kitu ili kufanikiwa akiwa na Madrid kabla ya mkataba wake kumalizika mwaka 2024.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
SPAIN
VERSUS
PORTUGAL
1 | 2.13
X | 3.24
2 | 3.44

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# SCALONI: ITALIA HAISTAHILI KUKOSA KOMBE LA DUNIA



**LONDON,** England

KOCHA wa Argentina, Lionel Scaloni amesema Italia haikustahili kukosa Kombe la Dunia, huku akiwa haoni kama Paulo Dybala akivurugwa na uvumi kuhusu mustakabali wake.

Washindi wa Euro 2020 Italia na mabingwa wa Copa America Argentina, jana Jumatano walikutana kwenye 'Finalissima' katika Uwanja wa Wembley nchini England.


Mchezo huo ulikuwa kati ya mabingwa wa bara la Amerika Kusini na wale wa bara la Ulaya.

Lakini hakuna nafasi ya wawili hao kukutana nchini Qatar Novemba kutokana na Italia kushindwa kufuzu kwa mara ya pili mfululizo katika Kombe la Dunia baada ya kufungwa katika mechi ya mtoano dhidi ya Macedonia Kaskazini, Machi.

Hilo lilisababisha maswali kuhusu mustakabali wa kocha Roberto Mancini na mfumo wa Italia kwa kushindwa kutoa wachezaji wachanga.

"Italia haikustahili kutokwenda Kombe la Dunia, bado ni mabingwa wa Ulaya, timu kubwa," alisema Scaloni akiwaambia waandishi wa habari. "Kuna michezo ambayo mpira hautaki kuingia langoni, na hivyo ndivyo michezo inavyopotea. Lakini Robert Mancini amefanya kazi kubwa, kurejesha utambulisho wa Italia baada ya miaka mingi.

"Sidhani atafanya mabadiliko mengi sasa, badala yake yatabadilika polepole kama tulivyofanya; hutokea kwa timu zote za taifa mapema au baadaye kwamba wanapaswa kubadilika. Sasa wanaweza kuanza upya."



# *Lewandowski azua balaa Laporta, rais wa Laliga*

**BARCELONA,** Hispania

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta amejibu maoni ya Rais wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Javier Tebas kwamba, 'Blaugrana' hao hawawezi kumudu kumsajili Robert Lewandowski.

Laporta amesema madai hayo ya Tebas yana nia ya kuiumiza Barcelona na kuharibu mipango yao.

Barca wanaonekana kuwa kwenye nafasi nzuri ya kumsajili nyota wa Bayern Munich, Lewandowski baada ya yeye mwenyewe kutangaza "muda wake umemaliza" akiwa na wababe hao wa Bundesliga.

Nyota huyo wa kimataifa wa Poland ameweka wazi upendeleo wake wa kutaka kujiunga na Barca, lakini Tebas alibainisha kuwa Blaugrana hao lazima wauze mmoja wa wachezaji wao wa thamani ili kuweza kukamilisha uhamisho huo.

"Barca tayari wanajua nini wanapaswa kufanya kama wanataka kumsajili Lewandowski," alisema Tebas akiiambia Europa Press Sports Breakfasts.

"Wanajua sheria zetu za udhibiti wa uchumi kikamilifu. Ni kuepuka matatizo makubwa ya kiuchumi. Sijui kama watamuuza (Frenkie) de Jong au Pedri.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# SERIKALI JICHO KWA SERENGETI GIRLS KUFUZU KOMBE LA DUNIA

**Na Saada Akida**

WAZIRI wa Utamaduni Sanaa na Michezo nchini, Mohammed Mchengerwa, amesema kwa kushirikiana na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), wamejipanga vizuri kuhakikisha Timu ya Taifa ya Wanawake chini ya miaka 17, (Serengeti Girls), inashinda mechi dhidi ya Cameroon ili kukata tiketi ya kushiriki Kombe la Dunia baadaye mwaka huu nchini India.

Serengeti Girls itaikaribisha Cameroon katika Uwanja wa Amaan visiwani Zanzibar Jumamosi wiki hii, huo ukiwa ni mchezo wa marudiano baada ya ule wa awali ugenini kuibuka na ushindi wa mabao 4-1.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mchengerwa alisema safari hii wamedhamiria kuhakikisha wanapambana timu za taifa zifanye vizuri huku wakiweka maandalizi sawa kuhakikisha Serengeti Girls inashinda.

**Alisema wizara yake itashirikiana bega kwa bega kuhakikisha wanasimamia na kuweka mipango madhubuti kwa timu hiyo kufanikiwa kucheza michuano ya Kombe la Dunia mwaka huu.**

"Mwaka huu tumedhamiria kuhakikisha tunaweka mipango sawa kwa kushirikiana na vyama, sasa hivi timu yetu ya Serengeti Girls imebakiza nafasi ndogo ya kwenda kucheza Kombe la Dunia," alisema Mchengerwa.

"Tunapambana iweze kutetema au kunyunyiza kuhakikisha vijana wetu wanapambana kushinda mchezo wetu wa Jumamosi ambao tukishinda tunaenda kucheza fainali za Kombe la Dunia," aliongeza Mchengerwa.

Timu itakayopata matokeo ya jumla Jumamosi kati ya Serengeti Girls na Cameroon, itafuzu moja kwa moja kushiriki fainali hizo zitakazofanyika nchini India Oktoba mwaka huu.

## WAPIGENI...



Mchezaji wa Timu ya Taifa ya Brazil aliyeichezea Kombe la Dunia mwaka 2002, Juliano Balletti (kushoto), akisalimiana na mchezaji wa Timu ya Taifa ya Tanzania, 'Taifa Stars', Salum Abubakar (Sure Boy), wakati alipowatembelea katika kambi yao ya mazoezi kwenye Uwanja wa Taifa wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam, jana, wakati huu ikijiandaa na mechi za kuwania kufuzu Afcon 2023 dhidi ya Niger na Algeria.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Diarra, Metacha wang'ara Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

KIPA wa Yanga raia wa Mali, Djigui Diarra, anaongoza kwa kucheza mechi nyingi bila kuruhusu bao 'clean sheets', kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara inayoelekea ukingoni, huku makipa watatu, Metacha Mnata wa Polisi Tanzania, Aboubakar Abbas wa Coastal Union na Hamad Kadedi wa Mbeya Kwanza wakiongoza kwa kuokoa mikwaju ya penalti.

Diarra, mpaka kufikia raundi ya 26 ya Ligi Kuu, timu zikibakisha mechi tano na zingine nne kumaliza ligi, ana 'clean sheets' 15 na kwa upande mwingine Metacha Mnata anaongoza kwa kuokoa penalti mbili mpaka sasa, akiwa kipa pekee aliyeokoa nyingi kuliko wengine.

Kwa mujibu wa takwimu za Ligi Kuu, kipa wa Simba, Aishi Manula anashika nafasi ya pili kwa 'clean sheets' nyuma ya Diarra akiwa nazo 11, kipa mwingine wa Yanga, Abdallah Mshery yeye akiwa nazo tisa, zingine akiwa ametoka nazo kwenye klabu yake ya zamani, Mtibwa Sugar, kabla ya kujiunga na timu hiyo kipindi cha dirisha dogo.

James Ssetuba wa Biashara United na Metacha wa Polisi Tanzania wao wamekaa golini mechi nane bila kuruhusu wavu wao kuguswa kila mmoja, kipa wa Mbeya Kwanza, Hamad Kadedi na Said Kipao wa Kagera Sugar wakiwa wana 'clean sheets' saba kila mmoja.

Metacha, Kadedi na Aboubakar wanaongoza kwa kuokoa penalti mbili kila mmoja, Ahmed Salula wa Azam FC, Mshery wa Yanga, Ssetuba wa Biashara United, na Mohamed Makaka wa Ruvu Shooting kila mmoja ameokoa penalti moja.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 02/06/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2663 | Japan vs Paraguay | 1.81 | 3.51 | 4.48 |
| 14:00 | 2867 | South Korea vs Brazil | 7.55 | 4.59 | 1.41 |
| 14:30 | 4232 | Ghana Youth vs Indonesia Youth | 1.21 | 5.31 | 11.80 |
| 16:00 | 2808 | South Korea U23 vs Malaysia U23 | 1.09 | 7.25 | 23.51 |
| 17:30 | 1952 | Arman Gohar Sirjan vs Machine Sazi Tabriz | 1.14 | 6.08 | 17.65 |
| 17:30 | 2825 | Esteghlal Khuzestan vs Khosheh Talaei | 1.51 | 3.43 | 6.86 |
| 17:30 | 3726 | Sanat Mes Kerman FC vs Pars Jonoubi Jam | 1.47 | 3.47 | 7.63 |
| 17:30 | 3971 | Shahrdari Hamedan vs Esteghlal Mollasani | 2.65 | 2.55 | 3.04 |
| 17:30 | 4046 | Vista Turbine vs Kheybar Khorramabad FC | 2.66 | 2.52 | 3.06 |
| 17:30 | 4327 | Ghasghaei Shiraz vs Shams Azar Qazvin | 2.79 | 2.33 | 3.19 |
| 17:30 | 5700 | Rayka Babol vs Saipa Karadj | 2.28 | 2.69 | 3.47 |
| 17:30 | 5878 | Latvia U21 vs Israel U21 | 5.91 | 4.24 | 1.44 |
| 17:30 | 5887 | Shahin Bushehr vs Malavan Bandar Anzali | 19.68 | 5.12 | 1.17 |
| 17:30 | 5990 | Shahrdari Astara vs Mes Shahr-e Babak | 2.25 | 2.42 | 4.11 |
| 18:00 | 3461 | Thailand U23 vs Vietnam U23 | 1.87 | 3.15 | 4.04 |
| 18:00 | 3728 | Macedonia U21 vs Armenia U21 | 1.45 | 4.22 | 5.70 |
| 18:30 | 2023 | Sepahan Esfahan vs Aluminium Arak | 1.56 | 3.34 | 6.28 |
| 18:30 | 3172 | Sanat Naft Abadan vs Havadar | 2.42 | 2.37 | 3.78 |
| 18:30 | 3411 | Fajr Sepasi vs Persepolis FC | 6.89 | 3.34 | 1.52 |
| 18:30 | 3614 | Padideh Mashhad vs Foolad Khuzestan | 5.72 | 2.81 | 1.76 |
| 18:30 | 4574 | Nurmijarven Jalkapalloseura vs Hps W | 4.80 | 4.31 | 1.52 |
| 18:30 | 4912 | Gol Gohar vs Zob Ahan | 1.97 | 2.64 | 4.70 |
| 18:30 | 5874 | FC San Pedro vs Bassam | 1.68 | 3.09 | 5.48 |
| 19:00 | 1353 | Mozambique vs Rwanda | 2.25 | 2.88 | 3.59 |
| 19:00 | 1440 | Cyprus vs Kosovo | 3.53 | 3.23 | 2.10 |
| 19:00 | 1827 | Bulgaria vs North Macedonia | 2.73 | 3.03 | 2.68 |
| 19:00 | 3635 | Estonia vs San Marino | 1.09 | 8.65 | 29.18 |
| 19:00 | 4084 | Georgia vs Gibraltar | 1.08 | 9.26 | 30.19 |
| 19:00 | 4460 | Kedainiai Nevezis vs Vmfd Zalgiris-3 | 1.63 | 3.83 | 4.42 |
| 20:00 | 2967 | Girona vs Eibar | 2.19 | 3.14 | 3.28 |
| 20:00 | 3498 | Bandirmaspor vs Istanbulspor | 2.17 | 3.34 | 2.95 |
| 20:00 | 3881 | Valur Reykjavik W vs IBV Vestmannaeyjar W | 1.10 | 7.86 | 15.71 |
| 20:00 | 4367 | Kjellerup IF vs Fuglebakken Kfum | 1.39 | 4.89 | 5.68 |
| 20:00 | 5185 | Ullensaker/Kisa vs Asker | 1.66 | 4.02 | 4.02 |
| 20:30 | 4969 | Luxembourg U21 vs Sweden U21 | 15.69 | 7.06 | 1.12 |
| 21:00 | 1846 | Racing Club Dabidjan vs ASEC Mimosas | 5.00 | 3.20 | 1.75 |
| 21:30 | 2416 | Fjolnir Reykjavik W vs Grindavik W | 2.75 | 4.13 | 2.02 |
| 21:30 | 5817 | San Marino U21 vs Poland U21 | 34.55 | 12.83 | 1.01 |
| 21:45 | 1726 | Israel vs Iceland | 1.86 | 3.53 | 4.03 |
| 21:45 | 1826 | France U21 vs Serbia U21 | 1.14 | 6.48 | 14.73 |
| 21:45 | 2449 | Slovenia vs Sweden | 3.23 | 3.13 | 2.26 |
| 21:45 | 2957 | Northern Ireland vs Greece | 3.13 | 2.98 | 2.41 |
| 21:45 | 3640 | Spain vs Portugal | 2.13 | 3.24 | 3.44 |
| 21:45 | 4398 | Serbia vs Norway | 2.24 | 3.18 | 3.23 |
| 21:45 | 4617 | Czech Republic vs Switzerland | 2.98 | 3.23 | 2.35 |
| 22:00 | 1165 | Tunisia vs Equatorial Guinea | 1.39 | 4.44 | 7.87 |
| 22:00 | 5212 | Cobreloa vs CD Santa Cruz | 1.71 | 3.48 | 4.41 |
| 22:15 | 5343 | Augnablik W vs FH Hafnarfjordur W | 9.02 | 6.27 | 1.21 |
| 23:00 | 1972 | Anguilla vs Dominica | 8.08 | 5.12 | 1.28 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Alhamisi Juni 2, 2022

Nipashe




'Italia haistahili kukosa Kombe la Dunia' UKURASA 22

# Nabi ataja wakusajili Yanga

●●● Asema lengo kuimarisha kikosi mapema kuelekea michuano ya CAF, ambapo...

**Na Saada Akida**

BAADA ya kujihakikishia nafasi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, ametaja maeneo anayotaka kuyaboresha kwenye kikosi chake ili kuweza kutoa ushindani mkubwa na kufika mbali katika michuano hiyo inayoongoza kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani humu.

**Yanga ambayo ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara, inahitaji alama tatu tu katika michezo minne iliyobakiza ili kutawazwa mabingwa wapya wa Ligi Kuu Bara msimu huu wa 2021/22.**

Hata hivyo, tayari ina tiketi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika kwani hata isipotwaa ubingwa huo ina uhakika wa kumaliza nafasi mbili za juu, hasa ukizingatia msimu ujao Tanzania itaingiza timu nne kwenye michuano ya kimataifa, mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema anatakiwa kuimarisha kikosi cha timu hiyo kuelekea mashindano ya kimataifa ili kutorudia makosa ya kutolewa katika hatua za awali msimu huu wa Ligi ya Mabingwa uliomalizika Jumatatu wiki hii.

Msimu huu wa Ligi ya Mabingwa Afrika ambao ulimalizika Jumatatu kwa Wydad Casablanca ya Morocco kutwaa ubingwa wa huo kwa kuifunga Al Ahly ya Misri mabao 2-0 kwenye mechi ya fainali, Yanga iliishia hatua ya awali baada ya kutolewa na Rivers United ya Nigeria kwa jumla ya mabao 2-0 kutokana na kufungwa bao 1-0 nyumbani na ugenini.

Lakini Nabi, ameanza kumulika mapema michuano hiyo kwa kutaka kukiboresha kikosi chake baada ya kulieleza gazeti hili maeneo ambayo anataka kuyaongezea nguvu ili kuweza kufika mbali pindi itakapoanza.

Nabi alisema usajili atakaoufanya utazingalia mapungufu yao hususan idara ya ulinzi na ushambuliaji, ambazo zinahitaji kuongezewa nguvu zaidi.

"Tunahitaji kufanya maboresho katika usajili wetu kwa kuongeza baadhi ya wachezaji watakaosaidia kufikia malengo katika michuano ya kimataifa, tunahitaji kuwa imara zaidi ili kuepuka fedheha kama msimu uliopita (ulimalizika)," alisema Nabi.

Alisema anahitaji beki wa maana wa kushoto ambaye atakuwa na sifa za kujua kuzuia na kupiga krosi kali zenye madhara kwa wapinzani, kwani kimataifa wanataka kuingia na miguu miwili msimu ujao.

Kocha huyo alisema msimu uliopita walifanya makosa ambayo hawataki kuyarudia safari hii kwa kuhakikisha timu hiyo inafanya vizuri katika michuano hiyo na kufika katika hatua ya makundi.

Kuelekea mechi nne zilizobakia, Nabi alisema malengo yao ni kuendelea walipoishia kwa kuhakikisha wanashinda katika michezo hiyo ili kuweka rekodi ya kumaliza ligi bila ya kufungwa.

Ligi hiyo kwa sasa imesimama kupisha mapumziko ya Kalenda ya Fifa, kwa timu za taifa kwa Ukanda wa Afrika kucheza mechi za kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2023, zitakazofanyika mwakani nchini Ivory Coast.

TUZO...



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, akimpa tuzo Msanii wa Muziki wa Hiphop nchini, Joseph Mbilinyi 'Sugu' ya kuthamini mchango wake katika sanaa na kuzalisha ajira kabla ya kuzindua kitabu cha msanii huyo chenye jina la Muziki na Maisha 'From the Street', katika Tamasha la Dream Concert lililofanyika Serena jijini Dar es Salaam usiku wa kuamkia jana. **PICHA: IKULU**

## Simba: Tumefanya maamuzi sahihi

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imesisitiza kuwa imefanya maamuzi sahihi na wakati sahihi kuachana na kocha wake raia wa Hispania Pablo Franco, ikiwa tayari imeanza mchakato wa kusaka mwalimu mpya, huku wakala wa Mhispania huyo, Mkenya Edgar Mitema, akisema mteja wake yuko kwenye mazungumzo na klabu ya Raja Casablanca ya Morocco.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally amesema jana kuwa, klabu hiyo imefanya maamuzi sahihi kwa sababu hakuna yeyote kati ya klabu na kocha huyo aliyefikia malengo.

"Yalikuwa ni makubaliano ya pande zote mbili, kila mmoja alikuwa na malengo yake na kila mmoja alimpa mwenzake malengo pia. Pablo hajakwama, ila pande zote mbili hazijatimiza malengo, Simba hatujatimiza na wala Pablo hajatimiza, sasa taasisi mbili zilizokubaliana kufanya kazi pamoja kama hazitatimiza malengo hakuna sababu ya kuendelea kuwa pamoja," alisema Ahmed.

Alisema kuwa hata muda walioamua kuachana na kocha huyo ni sahihi kwa sababu kila mmoja atakuwa na wakati mzuri wa kuangalia malengo yake ya baadaye kwa muda muafaka, tofauti na kama wangesubiri ligi imalizike.

Hata hivyo, kuna tetesi kuwa huenda kocha wa zamani wa APR ya Rwanda raia wa Morocco, Mohamed Adil Erradi akatwaa mikoba hiyo.

Naye wakala wa kocha Pablo, Mitema amesema si jambo la ajabu sana kwa makocha kutimuliwa kwenye klabu, lakini kwa mteja wake si kwamba hakutimiza malengo waliyokubaliana kwani moja ya vipengele anavyovifahamu vilivyokuwa kwenye mkataba ni kwamba atatimuliwa kama timu itafungwa mechi tatu mfululizo.

"Siyo mbaya, ataenda Raja Casablanca, ameitwa kufanya usaili kama mambo yataenda vizuri, basi atakuwa kocha nchini Morocco," alisema.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042